# HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA

## SHULE YA MSINGI RWENSINGA

**JARIBIO LA SOMO HISABATI DARASA LA VII JUMATATU 20.01.2022**

1 Ipi kati ya sehemu zifuatazo ni sehemu rahisi ya 45%?
(a)$^9/_2$ (b)$^2/_9$ (c)$^9/_{20}$ (d)$^{20}/_9$ (e)$^{45}/_{10}$ [ ]

2 Namba ya Kirumi inayowakilisha 49 ni
(a) LXIX (b) XVIX (c) XLIX (d)LVXI (e) XLXI [ ]

3 Chausiku ana shilingi 9,000. Amepungukiwa na asilimia ngapi ya fedha ili kununua katoni moja yenye chupa 24 za juisi, iwapo chupa moja ya juisi huuzwa kwa bei ya shilingi 500? (a) 75% (b) 33.3% (c) 25% (d) 50% (e) 66.7% [ ]

4 Kazimoto alichagua wanafunzi watano ili waandike kipeuo cha pili cha jumla ya namba witiri zilizopo kuanzia 1 hadi 11. Je, lipi ni sahihi kati ya majibu yafuatayo?
(a) 2 (b) 3 (c) 4 (d) 5 (e) 6 [ ]

5 Wanafunzi watano walipewa tarakimu 1, 3, 8, 9, 2, 4, 5 ili waunde namba nzima kubwa kuliko zote kwa kutumia tarakimu hizo. Je, ni namba ipi iliyoundwa ambayo ni kubwa kuliko nyingine? (a) 9,834,521 (b) 9,843,521 (c) 9,853,421 (d) 9,854,321 (e) 9,845,321 [ ]

6 Shule ilikusanya ada shillingi 39,076. Katika makusanyo haya ni tarakimu ipi inawakilisha mamia?
(a) 6 (b) 3 (c) 0 (d) 7 (e) 9 [ ]

7 Matokeo ya uchaguzi wa viongozi uliofanyika shuleni yalikuwa kama ifuatavyo; Zawadi alipata kura 876, Baraka kura 718 na Waridi kura 561. Tofauti ya kura nyingi zaidi na ndogo zaidi ni ipi kwa namba za Kirumi? (a) DLXI (b) CLVII (c) CLVIII (d) DCCXVIII (e) CCCXV [ ]

8 Wanafunzi watano walishindana kukimbia mbio awamu 3 kwa kupunguza hatua 6 kwa kila awamu. Iwapo walianzia hatua ya 59, yupi alimaliza awamu zote kwa mpangilio sahihi? (a) 59, 53, 47, 41 (b) 59, 65, 71, 78 (c) 59, 53, 41, 35 (d) 59, 65, 78, 84 (e) 59, 53, 47, 31 [ ]

9 Upi ni mpangilio sahihi wa kupungua wa namba witiri zilizopo kati ya 50 na 60? (a) 61, 59, 57, 55, 53 (b) 59, 57, 55, 53, 51 (c)58, 56, 54, 52, 50 (d)59, 53 (e)59, 58, 57, 56, 55, 54, 53, 52, 51 [ ]

10 Shule tatu R, S na T ziligawana dazeni 120 za vitabu kama ifuatavyo; R alipata $^1/_3$ ya vitabu vyote na S alipata 60% ya vitabu vilivyobaki. Ikiwa vitabu vilivyobaki vilikuwa vya Shule T. Je, shule T ilipata vitabu vingapi?
(a) 480 (b) 576 (c) 120 (d) 384 (e) [ ]

11

Mwalimu alichagua wanafunzi watano ili kupanga namba zifuatazo 0.04, 2%, $^1/_4$, 1 na $^-2$. Upi ni mpangilio sahihi kati ya ifuatayo? (a) 1, $^1/_4$, $^-$ 2, 0.04, 2% (b) $^-2$, 1, 0.04, 2%, $^1/_4$ (c) $^-2$, 2%, 0.04, $^1/_4$, 1 ... 1, $^1/_4$

MsomiBora.

12

Ni namba ipi ina... namba zifuatazo? 17, 21, 25, 29, ______
13 (a) 37 (b) 33 (c) 28 (d) 30 (e) 43 [ ]
Ipi ni namba ndogo kuliko zote katika seti ya namba zifuatazo? { 0.75, $^-$ 1, 0.5, 0, $^-$ $^3/_4$ }
(a) 0 (b) 0.5 (c) 0.75 (d) $^-1$ (e) $^-3/_4$ [ ]

14

Nini thamani ya $^-15$ x ( $^-14$ + 8 )?
(a) $^+90$ (b)$^-37$ (c) $^-90$ (d) $^+330$ (e)$^-330$ [ ]

15

Je, kuna 0.36 ngapi katika 1$^4/_5$? (a)50 (b)2 (c)5 (d)20 (e)500 [ ]

16

Nini zao la 0.9 na 3.21? (a) 2.889 (b) 2.789 (c) 28.89 (d) 2.31 (e) 4.11 [ ]

17

Josephine huuza kuku 60 kila mwezi kwa faida ya Shilingi 3,000 kwa kila kuku. Je, kwa mwaka mmoja Josephine hupata faida ya kiasi gani kutokana na biashara hiyo? (a) 21,600,000 (b) 2,160,000 (c) 720,000 (d) 36,000 (e) 180,000 [ ]

18

Tafuta thamani ya 4$^4/_5$ ÷ 48 = (a) $^1/_5$ (b) $^1/_{10}$ (c) $^1/_2$ (d) $^{10}/_1$ (e) $^1/_{100}$ [ ]

19

Mwalimu aliwapa wanafunzi kazi ya kutafuta thamani ya mtajo 8 – ($^-3$ + $^+8$). Je, ni lipi jibu sahihi walilopata? (a)$^-3$ (b) $^+19$ (c) $^+13$ (d) $^+3$ (e) 13 [ ]

20

Wazazi wa watoto watatu Asha, Juma na Jamila walikuwa na kiasi cha fedha kama ifuatavyo: Mzazi wa Asha Sh. 1,039,000, mzazi wa Juma Sh. 929, 000 na mzazi wa Jamila Sh. 820,000. Kama wazazi wa Juma na Jamila wangeunganisha fedha zao, wangemzidi mzazi wa Asha kwa kiasi gani cha fedha? (a)Sh 710,000 (b)Sh 601,000 (c)Sh 611,000 (d)Sh 619,000 (e)Sh 219,000 [ ]

21

Bwana Ngasa alivuna mazao yafuatayo; maharage magunia 20, mahindi magunia 60, mpunga magunia 50 na karanga magunia 30. Ikiwa aliuza $^1/_5$ ya magunia ya kila zao, je, aliuza magunia mangapi ya mazao yote? (a)Magunia 42 (b)Magunia 32 (c)Magunia 22 (d)Magunia 12 (e)Magunia 28 [ ]

22

Shamba la ng'ombe wa maziwa huzalisha lita 254,567 za maziwa kwa siku. Ni kiasi gani cha maziwa kitazalishwa kwa siku 43? (a)Lita 10,646,381 (b)Lita 10,945,381 (c)Lita
23 10,946,381 (d)Lita 10,846,381 (e)Lita 10,746,381 [ ]

Garimoshi liliondoka Arusha saa 5 na dakika 10 asubuhi na kutumia muda wa saa 15 na dakika 15 kufika jijini Dar es Salaam. Je, garimoshi hilo lilifika Dar es Salaam saa ngapi? (Jibu liwe katika utaratibu wa saa 12). (a)8:25 usiku (b)8:25 adhuhuri (c)2:25 usiku (d)2:25 asubuhi
24 (e)3:15 usiku [ ]

Viwanja vinne vya makazi viliuzwa kwa jumla ya shilingi 5,500,000. Ikiwa viwanja vitatu viliuzwa kwa shilingi 1,257,000 kila kimoja, je, kiwanja cha nne kiliuzwa kwa
25 shilingi ngapi? (a)sh 1,375,000 (b)sh 2,632,000 (c)sh 2,989,000 (d)sh 3,771,000 (e)sh 1,729,000 [ ]


Gawanya miaka 95 na miezi 8 kwa 28.
(a)Miaka 3 na miezi 0 (b)Miaka 3 na miezi 5 (c)Miaka 5 na
26 miezi 3 (d)Miaka 3 na miezi 4 (e)Miaka 5 na miezi 4 [ ]

Jumla ya saa 6 na dakika 30 na saa 3 na dakika 45 ni ipi? (a)Saa 9 na dakika 75 (b)Saa 9 na dakika 15 (c)Saa 10 na dakika 05 (d)Saa 10 na dakika 25 (e)Saa 10 na
27 dakika 15 [ ]

Ni nini tofauti ya saa 8 dakika 20 na saa 5 dakika 45 (a)Saa 14 na dakika 05 (b)Saa 2 na dakika 75 (c)Saa 2 na dakika 35 (d)Saa 3 na dakika 25 (e)Saa 13 na
28 dakika 65 [ ]


Miaka 2015, 2016, 2017, 2018 na 2019 ni muda waliozaliwa watoto katika familia tano tofauti. Upi ni mwaka mrefu?
29 (a) 2015 (b) 2016 (c) 2017 (d) 2018 (e) 2019 [ ]

Jamali alipewa picha ya umbo la pembe tano lenye ukubwa wa pembe kama ilivyooneshwa kwenye Kielelezo Na. 1. Kama mtaalamu wa Hisabati, ipi kati ya zifuatazo ni thamani ya y?





(a) 2
(b) 20
(c) 4 [ ]
(d) 38
30 (e) 88

Juma alipewa kazi ya kujenga banda la kuku na akalijenga kama linavyoonekana katika umbo lifuatalo: Kama mtaalamu wa maumbo ya kihisabati, umbo hili linaitwaje?
(a)Pembetatu pacha
(b)Pembetatu mraba
(c)Pembetatu sawa
(d)Pembetatu gun
31 (e)Pembetatu sambamba



Mandalu alipanga kutumia siku 3 kujaza tenki la maji lenye kipenyo cha m 14 na kimo cha m 5. Ikiwa hujaza $m^3$ 154 za maji katika tenki hilo kwa siku. Je, siku ngapi zaidi zitahitajika kujaza tenki zima? (Tumia $\pi = {}^{22}/_{7}$).
32 (a) 2 (b) 5 (c) 4 (d) 6 (e) 7 [ ]

Ikiwa eneo la trapeza ABCD ni $sm^2$ 160, upi ni urefu wa BE?




(a) Sm 8
(b) Sm 10
(c) Sm 5 [ ]
(d) Sm 20
33 (e) Sm 13

Mwajuma alipewa kipande cha nguo chenye urefu wa dekameta $7^1/_4$. Urefu huo ni sawa na meta ngapi za kitambaa? (a)m 725 (b)m 7.25 (c)m 72,500 (d)m 72.5
34 (e)m 7,250 [ ]

Mzazi wa Kinje na Mzazi wa Kelo kwa pamoja walinunua kg 189 g 600 za sukari. Ikiwa waligawana sukari hiyo kwa kiwango kinacholingana, je, ni kiasi gani cha sukari kila mzazi alipata? (a) kg 90 g 375 (b) kg 94.5 g 300
35 (c) kg 94 g 350 (d) kg 94 g 800 (e) kg 94 g 300 [ ]

Chupa ya maji ina ujazo wa ml 350. Je, katoni 2 za chupa za maji zina jumla ya lita ngapi ikiwa kila katoni ina chupa 24? (a)lita 1.68 (b)lita 168 (c)lita 1,680 (d)lita 16.8
36 (e)lita 0.168 [ ]

Maganga hutembea umbali wa km 4 m 8 sm 12 kwa siku moja. Je, atatembea umbali gani kwa siku 15? (a)km 61 m 21 sm 80 (b)km 61 m 21 sm 180 (c)km 60 m 80 sm 20 (d)km
37 60 m 20 sm 80 (e)km 60 m 121 sm 80 [ ]

Ikiwa nyuzi za umbo lenye pembe nne ni $3t – 10^0$, $2t + 25^0$, $45° – t$ na $4t + 60^0$. Thamani ya herufi t katika umbo hilo ni
38 ipi? (a)15° (b)30° (c)60° (d)90° (e)120° [ ]

Kiwanja cha mpira wa miguu kina mzingo wa mita 112. Ikiwa urefu wa kiwanja hicho ni Meta (x – 2) na upana wake ni Meta ( $2^1/_2 x - 5$), thamani ya *x* itakuwa ngapi?
39 (a) 56 (b) 98 (c) 18 (d) 14 (e) 42 [ ]

Darasa lina jumla ya wanafunzi 9. Wastani wa uzito wa wanafunzi 5 ni kilogramu 20. Tafuta jumla ya uzito wa wanafunzi wote ikiwa wastani wa uzito wa wanafunzi waliobaki ni kilogramu 30. (a) Kilogramu 50 (b) Kilogramu 450 (c)Kilogramu 100 (d)Kilogramu 220
40 (e)Kilogramu 130 [ ]

Ikiwa wastani wa sh 100, sh 250, sh 350 na sh 3p ni sh 205, thamani ya herufi 'p' itakuwa ngapi? (a) 40 (b) 120 (c) 85 (d) 165 (e) 161 [ ]

41

## SEHEMU B:

## MATENDO YA KIHISABATI, MAUMBO NA MAFUMBO


Idadi ya wanafunzi waliohitimu Darasa la Saba mwaka 2018 katika Kata yetu ilikuwa 600. Kati ya hao, $7^1/_2$% hawakufaulu mtihani. Je, ni sehemu gani ya wahitimu walifaulu mtihani?

42

Peo tatu za shamba lenye umbo la mstatili ni A ( $^{-}4$, 1 ), B ( $^{-}4$, $^{-}2$ ), na C ( 3, $^{-}2$ ). Tumia grafu ya majira ya nukta kutafuta peo ya nne.

43

Kijiji cha Mtakuja kilitaka kujenga Zahanati katika kiwanja kinachowakilishwa na umbo lifuatalo:




Je, kiwanja hicho kina eneo kiasi gani katika meta za mraba?

44

Katika shule ya msingi Railway, mwanafunzi akipata daraja A katika somo lolote, mmiliki wa shule humlipa mwalimu shilingi 10,000 kwa kila A kama motisha kwenye somo lake. Ikiwa mwalimu wa Hisabati alipata shilingi 1,250,000, je ni wanafunzi wangapi walipata daraja A katika somo hilo?

45

Bahati alikuwa na kalamu 8 na penseli 12. Aliamua kuwagawia rafiki zake kalamu 3 na penseli 5. Iwapo aliuza idadi ya kalamu zilizobaki kwa shilingi 200 kila moja, penseli zilizobaki kwa shilingi 100 kila moja, je, alipata jumla ya kiasi gani cha fedha?

MsomiBora.com

# MAJIBU YA JARIBIO

## SOMO LA HISABATI – DARASA LA VII

<table>
<tr><th>Na</th><th>Jibu</th><th>Na</th><th>Jibu</th><th>Na</th><th>Jibu</th></tr>
<tr><td>1</td><td>C</td><td>21</td><td>B</td><td rowspan="4">41</td><td rowspan="4">$^{111}/_{120}$<br>(Wanafunzi 555)</td></tr>
<tr><td>2</td><td>C</td><td>22</td><td>C</td></tr>
<tr><td>3</td><td>C</td><td>23</td><td>A</td></tr>
<tr><td>4</td><td>D</td><td>24</td><td>E</td></tr>
<tr><td>5</td><td>D</td><td>25</td><td>B</td><td rowspan="4">42</td><td rowspan="4">$D(^{+}3, ^{+}1)$</td></tr>
<tr><td>6</td><td>C</td><td>26</td><td>E</td></tr>
<tr><td>7</td><td>E</td><td>27</td><td>C</td></tr>
<tr><td>8</td><td>A</td><td>28</td><td>B</td></tr>
<tr><td>9</td><td>B</td><td>29</td><td>B</td><td rowspan="4">43</td><td rowspan="4">Meta$^2$ 215</td></tr>
<tr><td>10</td><td>D</td><td>30</td><td>C</td></tr>
<tr><td>11</td><td>A</td><td>31</td><td>C</td></tr>
<tr><td>12</td><td>B</td><td>32</td><td>B</td></tr>
<tr><td>13</td><td>E</td><td>33</td><td>D</td><td rowspan="3">44</td><td rowspan="3">Wanafunzi 125</td></tr>
<tr><td>14</td><td>A</td><td>34</td><td>D</td></tr>
<tr><td>15</td><td>C</td><td>35</td><td>D</td></tr>
</table>

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 16 | A | 36 | E | | |
| 17 | B | 37 | B | 45 | Sh. 1700/= |
| 18 | B | 38 | C | | |
| 19 | A | 39 | D | | |
| 20 | A | 40 | B | | |

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA

**SHULE YA MSINGI RWENSINGA**

**JARIBIO LA SOMO KISWAHILI DARASA LA VII JUMANNE 20.01.2022**

**SEHEMU A: SIKILIZA KWA MAKINI HADITHI UTAKAY-OSOMEWA NA MSIMAMIZI.KISHA JIBU SWALI LA 1 – 5**

1. **Adabu alikuwa Kiongozi mwenye tabia gani kati ya zifuatazo? ________ (a)Mwongo na shupavu (b)Shupavu na mwoga (c)Mkakamavu na mvivu (d)Shupavu na mzalendo (e)Mpenda raha sana [ ]**
2. **Kwa nini Adabu alipendwa na Wanakijiji? ______________ (a)Alipenda haki (b)Aliua simba (c)Alikuwa na mshale (d)Alikuwa na nguvu (e)Alikuwa msomi [ ]**
3. **Nani alipiga kelele akisema tumevamiwa na simba? ____ (a)Wanakijiji (b)Mzee Funzi (c)Kijana (d)Adabu (e)Kiongozi**
4. **Kwa nini Adabu aliwagawa wanakijiji katika makundi mawili? _______ (a)Wamfukuze simba (b)Wamuue simba (c)Wamuone simba (d)Wamtege simba (e)Wamtishie simba**
5. **Je unapata funzo gani kutokana na hadithi uliyoisikiliza? ________ (a)Tunapaswa kushirikiana (b)Ni lazima kumpiga simba (c)Ni vizuri watu kukusanyika (d)Tunapaswa kubeba silaha (e)Ni lazima kumuua simba [ ]**
6. **Mtu asiyepokea ushauri wa wengine huishia kuharibikiwa katika maisha. Ni methali ipi kati ya zifuatazo itafaa kufikisha ujumbe huu? _______ (a)Asiyekuwepo machoni na moyoni hayupo. (b)Asiyesikia la mkuu huvunjika guu. (c)Asiye na mengi ana machache. (d)Asiyeangalia huishia ningalijua. (e)Asiyeuliza hana ajifunzalo [ ]**
7. **"Mama alimwagiza Chitemo, "Nenda ukanunue mboga za majani." Sentensi hii ipo katika kauli ipi kati ya zifuatazo? __ (a)Taarifa (b)Mazoea (c)Halisi (d)Tata (e)Mbiu [ ]**
8. **Katika maneno yafuatayo neno lipi halilandanina mengine? ________________________ (a)Ndovu (b)Mbogo (c)Faru (d)Korongo (e)Nyumbu [ ]**
9. **"Akibeba watoto hawezi kuwashusha." Maana ya kitendawili hiki ni sawa na kitendawili kipi kati ya hivi? _____ (a)Hausimami hausimiki (b)Mjomba hataki tuonane (c)Pazia la Mungu (d)Bomu la machozi (e)Babu amelala ndani ndevu ziko nje. [ ]**
10. **Tumemsikia Nadi akisema, "Mimi huwa ninapenda kusoma jioni." Sentensi ipi kati ya zifuatazo inatoa taarifa ya alichokisema Nadi? ____ (a)Nadi alisema kuwa yeye huwa anapenda kusoma jioni. (b)Nadi alisema kuwa mimi huwa napenda kusoma jioni. (c)Nadi alisema kuwa yeye alikuwa anapenda kusoma jioni. (d)Nadi alisema kuwa mimi nilikuwa ninapenda kusoma jioni (e)Nadi alisema kuwa weweunapenda kusoma jioni. [ ]**
11. **Migodela alipopata taarifa ya msiba,alirudi nyumbani na kukuta msiba umekwisha. Ni nahau gani inaweza kutumika kueleza hali hiyo kati ya hizi? ______________ (a)Kaa kitako (b)Anua matanga (c)Enda jongomeo (d)Kusanya virago (e)Kata shauri. [ ]**
12. **Katika sentensi "Shangazi alimwambia kuwa atakapopata nauli atakuja kijijini", mzungumzaji ametumia nafsi gani kati ya hizi? ________________________ (a)Nafsi ya pili wingi (b)Nafsi ya tatu wingi (c)Nafsi ya tatu umoja (d)Nafsi ya pili umoja (e)Nafsi ya kwanza wingi [ ]**
13. **Selule ni kijana mchapakazi hodari aliyelima bustani kubwa ya mboga za majani kisha kuuza na kujipatia fedha za kutosha. Ni methali ipi kati ya hizi inafaa kuelezea hali hii? _____________________ (a)Simba mwenda pole ndiye mla nyama. (b)Mchumia juani hulia kivulini (c)Mwenda tezi na omo marejeo ngamani. (d)Mpanda hovyo hula hovyo. (e)Mla mla leo mla jana kala nini? [ ]**
14. **Babu alisema "Kilimo ni uti wa mgongowa taifa letu." Je babu alimaanisha nini kati ya yafuatayo? _____________ (a)Kilimo hakitegemewi (b)Kilimo kinategemewa (c)Kilimo hakifurahishi (d)Kilimo kinafurahisha (e)Kilimo kinachosha**
15. **"Afadhali jirani mchawi _________." Ni kifungu kipi kati ya vifuatavyo kinakamilisha methali hii kwa usahihi? (a)kuliko mlevi (b)kuliko mjeuri (c)kuliko mmbea (d)kuliko mwongo (e)kuliko mnafiki [ ]**
16. **"Nyafu alipotoka kazini alianza kukata maji hadi usiku wa manane." Je Nyafu alifanya nini kati ya mambo yafuatayo? __ (a)Alikunywa uji (b)Alikunywa chai (c)Alikunywa pombe (d)Alikunywa maziwa (e)Alikunywa maji [ ]**
17. **Pembua ana tabia ya kumwaga chakula kinachobaki baada ya kushiba. Je utatumia methali ipi kati ya zifuatazo kumshauri Pembua aache tabia hiyo? _______________ (a)Nyongeza haigombi. (b)Mwenye shibe hamjui mwenye njaa. (c)Akiba haiozi. (d)Haba na haba hujaza kibaba. (e)Usiache mbachao kwa msala upitao [ ]**
18. **Baba yangu ni "MHADHIRI" wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Je, Baba yangu anafanya kazi gani kati ya hizi zifuatazo? _____ (a)Anasoma masomo ya Chuo Kikuu (b)Anasajili wanafunzi wa Chuo Kikuu (c)Anafundisha wanachuo wa Chuo Kikuu (d)Anafuatilia nidhamu ya wanachuo (e)Anahudumia wageni katika Chuo [ ]**
19. **Alaa! Kumbe umekuja kwangu leo? Katika sentensi hii neno lililotumika kama kihisishi ni lipi kati ya yafuatayo? _ (a)umekuja (b)kumbe (c)leo (d)alaa! (e)kwangu [ ]**
20. **"Kabwela amefiwa na wazazi wake wote wawili." Je, Kabwela atakuwa na sifa ipi kati ya zifuatazo? ___ (a)Yatima (b)Mgane (c)Mjane (d)Muathirika (e)Mpweke**
21. **"Mjomba alikwenda kumuona bibi kijijini." Ni neno lipi kati ya yafuatayo limetumika kama kielezi katika sentensi hii? ____ (a)bibi (b)alikwenda (c)mjomba (d)kijijini (e)kumuona.**

22. **“Ninakwenda sokoni.”Sentensi hii ipo katika kauli gani kati ya zifuatazo? ______________________________ (a)Tata (b)Taarifa (c)Halisi (d)Masharti (e)Ombi [ ]**
23. **Wingi wa sentensi “nimeamua kusoma kwa bidii” ni upi kati ya sentensi zifuatazo? _____ (a)Wameamua kusoma kwa bidii (b)Umeamua kusoma kwa bidii (c)Mmeamua kusoma kwa bidii (d)Tumeamua kusoma kwa bidii (e)Ameamua kusoma kwa bidii [ ]**
24. **Methali ipi hutumika kumuonya mtu asiyesikiliza ushauri wa wakubwa? _____ (a)Hakuna masika yasiyokuwa na mbu (b)Asiyesikia la mkuu huvunjika guu (c)Asiyekuwepo na lake halipo. (d)Akupaye kisogo sio mwenzako. (e)Kidole kimoja hakivunji chawa [ ]**
25. **Kukiwa kuna shida ndogo itatuliwe mapema kabla haijawa kubwa. Methali ipi inahusiana na kifungu hicho cha maneno kati ya hizi? ______________________________ (a)Hauchi hauchi unakucha (b)Mwanzo wa ngoma ni lele (c)Usipoziba ufa utajenga ukuta (d)Penye miti hapana wajenzi. (e)Fimbo ya mnyonge ni umoja [ ]**
26. **Mashaka ni mtu asiyependa kutunza vitu kwa manufaa ya baadaye. Ni methali ipi kati ya zifuatazo itamsaidia kubadili mwenendo wake? ______________________ (a)Akili ni nywele (b)Akiba haiozi (c)Abwebwaye hujishika (d)Adui mpende. (e)Ahadi ni deni [ ]**
27. **Jogoo washamba ______ Kifungu kipi cha maneno kinaka-milisha kwa usahihi methali hiyo? (a)hawiki mjini (b)huwika mjini (c)huwika alfajiri (d)huliwa mjini (e)hawiki jioni**
28. **Bute anapenda kudadisi sana ili kuelewa jambo. Methali ipi kati ya zifuatazo inaelezea umuhimu wa tabia ya Bute? ______________________ (a)Asiye na bahati habahatishi (b)Asiyesikia la mkuu huvunjika guu (c)Asiye na mengi ana machache (d)Asiyeuliza hana ajifunzalo (e)Asiyefahamu urafiki si rafiki [ ]**
29. **“Bandu bandu humaliza gogo.” Methali ipi kati ya zifuatazo inafanana na hii? __________ (a)Pole pole ndio mwendo. (b)Mtaka cha uvunguni sharti ainame. (c)Samaki mkunje angali mbichi. (d)Chovya chovya humaliza buyu la asali. (e)Mtaka yote kwa pupa hukosa yote [ ]**
30. **Mwalimu Kaze aliwapa wanafunzi wake maswali ya chemshabongo. Nahau “chemshabongo” kama ilivyotumika katika sentensi hii ina maana gani kati ya zifuatazo? ____ (a)Changamsha akili (b)Fikiri kwa makini (c)Sumbua akili (d)Fikiri sana (e)Amsha ubongo [ ]**
31. **Uongozi wa mtaa ulivalia njuga tatizo la uporaji. Nahau “valia njuga” kamailivyotumika katika sentensi hii ina maana gani? _____________ (a)Kufuatilia kwa jazba (b)Kufuatilia kwa hasira (c)Kufuatilia kwa makini (d)Kufuatilia kwa siri (e)Kufuatilia kwa tahadhar [ ]**
32. **Mama alipanga vyombo kabatini. Kinyume cha neno “panga” ni lipi kati ya yafuatayo? __________ (a)pangisha (b)pangusa (c)pangua (d)panua (e)pango [ ]**
33. **Babu yangu analima mashamba kwa ustadi. Nomino ipi inatokana na kubadilishwa kwa kitenzi “lima”? ________ (a)Limisha (b)Limiana (c)Limika (d)Mkulima (e)Kalime [ ]**
34. **Neno linalotokana nakudondosha silabi moja katika neno “sabuni” ni lipi kati ya yafuatayo? ___________________ (a)suna (b)buni (c)bunia (d)ibua (e)nusa [ ]**
35. **Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aling’atuka madarakani. Katika sentensi hii, kisawe cha neno “NG’ATUKA” ni kipi kati ya vifuatavyo? _____ (a)Kujiuzulu (b)Kustaafu (c)Fukuzwa kazi (d)Kustaafishwa (e)ng’atua**

**SEHEMU B: KWA KUTUMIA MANENO YALIYOMO KWENYE KISANDUKU KAMILISHA BARUA IFUATAYO KWAKUJIBU SWALI LA 36 – 40**

| |
|---|
| **Baraka Kazingumu, M. Tumaini, Nakutakia utekelezaji mwema, S. L. P 21, YAH. KUPANDISHWA CHEO NA KUBADULISHIWA MAJUKUMU** |

**36.__________**
**Nachingwea.**

**04.10.2020**

**37.________________________**
**Shule ya Msingi Kisovu,**
**S. L. P 41,**
**Namtumbo.**

**Ndugu,**

**38.______________________________**

**Rejea kichwa cha habari hapo juu.**

**Napenda kukujulisha kuwa kutokana na utendaji kazi wako mzuri umepandishwa cheo kutoka Mwalimu wa Michezo kuwa Afisa Utamaduni na Michezo wa Wilaya ya Kwetu kuzuri. Hivyo, unatakiwa kuhamia Makao Makuu ya Wilaya punde upatapo barua hii na utawajibika kwa nafasi hiyo.**

**39.________________________**
**40.________________________**

**Masumbuko Tumaini**
**Mkurugenzi**

**SEHEMU C: UFAHAMU SOMA KWA MAKINI HABARI IFUATAYO KISHA JIBU SWALI 41 - 45**

***Kachiku ni kijana mwenye tabia nzuri anayeishi na wazazi wake katika mtaa wa Kibaoni. Alibahatika kuzaliwa peke yake katika familia ya kitajiri. Wazazi wake walimpenda na kumdekeza sana, walimsomesha katika shule nzuri yenye gharama kubwa kwa lengo la kupata elimu bora.***

***Tabia ya Kachiku ilianza kubadilika kutokana na kuambatana na makundi mabaya shuleni. Kachiku alitumia muda mwingi sana kuzurura mitaani na vijiweni badala ya kusoma. Aliamini kwamba utajiri wa wazazi wake ni nguzo katika maisha yake, akasahau kwamba; “mtegemea cha nduguye hufa maskini. ”Hatimaye, tabia ya Kachiku ikakithiri akaanza kulewa na kuvuta***

***sigara. Unywaji wapombe ulipomkolea akaanza kukwapua vitu vidogovidogo nyumbani kwao ili apate fedha ya kukata maji. Aidha, alikuwa akirudi nyumbani akiwa amelewa chakari. Tabia hiyo haikuwafurahisha wazazi wake. Walijitahidi kumkanyana kumweleza madhara yake lakini alikaidi kama ilivyo ada "sikio la kufa halisikii dawa."Hakupenda kuwasikiliza wazazi wake na aliona kama wanampotezea muda.***

***Kadiri siku zilivyozidi kwenda ndivyo tabia ya Kachiku ilivyozidi kuwa mbaya. Akaanza kuvunja nyumba za watu na kuiba mali zao. Siku moja, Kachiku na wenzake walikwenda kuiba duka la jirani yao. Kwa bahati walikamatwa na askari aliyekuwa doria. Wazazi wa Kachiku walipigwa na butwaa baada ya kupata taarifa za kukamatwa kwa kijana wao. Kesi ilisikilizwa mahakamani na mwishowe Kachiku alihukumiwa kifungo cha miaka mitano jela.***

41. **Kichwa cha habari hii kingefaa kuwa kipi? ____________**
42. **Kutokana na habari uliyoisoma ni tabia gani mbaya alizokuwa nazo Kachiku? Taja mbili.**
    **________________________, ______________________**
43. **Nini maana ya neno "kanya" kama lilivyotumika katika habari uliyoisoma? ________________________________**
44. **Kwanini Kachiku alihukumiwa kifungo cha miaka mitano jela? ______________________________________**
45. **Unapata funzo gani kutokana na habari uliyoisoma?**
    **_____________________________________________**

# HADITHI

*Hapo zamani za kale palikuwa na kijiji kiitwacho Faru. Faru ni kijiji kilichokuwa karibu na msitu mkubwa wenye wanyama wakali. Wanakijiji wa Faru waliishi maisha ya raha sana. Kiongozi wao aliitwa Adabu, alikuwa kiongozi shupavu na mzalendo. Wanakijiji walimpenda kwa sababu alikuwa anajitoa kwa ajili ya kijiji chake, alipenda haki na alipigania maendeleo ya kijiji chake.*

*Siku moja Adabu akiwa nyumbani kwake alisikia kelele nje ya nyumba yake. Alipotoka nje aliona kundi kubwa la wanakijiji wameshikilia silaha mbalimbali kama vile rungu, sime na magongo, hakujua ni ya kazi gani? Akauliza kwa shauku "kuna nini?" Mzee Funzi akajibu kwa hofu "tumevamiwa! tumevamiwa! na simba. "Simba?" Adabu aliuliza huku akikimbia kurudi ndani, akatoka na mshale.* ***Punde si punde*** *ilisikika ngurumo nyuma ya nyumba yake.*

*Adabu akawaambia "Msiogope" kisha akawagawa katika makundi mawili ili kumzunguka na kumshambulia simba. Baada ya kukuru kakara za muda mrefu wanakijiji walifanikiwa kumuua simba. "Ama kweli* ***jifya moja haliinjiki chungu****," alisikika akisema kijana mmoja. Wanakijiji waliondoka kwa furaha na kila mmoja alirudi nyumbani. Mpaka sasa wanakijiji wa Faru wanaishi kwa amani na ushirikiano.*

# MAJIBU YA JARIBIO

## SOMO LA KISWAHILI – DARASA LA VII

| Na | Jibu | Na | Jibu | Na | Jibu |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | 21 | | 41 | |
| 2 | | 22 | | | |
| 3 | | 23 | | | |
| 4 | | 24 | | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 5 | | 25 | | 42 | |
| 6 | | 26 | | | |
| 7 | | 27 | | | |
| 8 | | 28 | | | |
| 9 | | 29 | | 43 | |
| 10 | | 30 | | | |
| 11 | | 31 | | | |
| 12 | | 32 | | | |
| 13 | | 33 | | 44 | |
| 14 | | 34 | | | |
| 15 | | 35 | | | |
| 16 | | 36 | | | |
| 17 | | 37 | | 45 | |
| 18 | | 38 | | | |
| 19 | | 39 | | | |
| 20 | | 40 | | | |

# KYERWA DISTRICT COUNCIL

## RWENSINGA PRIMARY SCHOOL

## ENGLISH LANGUAGE SUBJECT STANDARD VII Jan 20, 2022

**SECTION A: LISTEN CAREFULLY TO THE PASSAGE READ BY INVIGILATOR AND THEN ANSWER THE QUESTIONS THAT FOLLOW**

1. What is the Nusura‟s father occupation? _________ (a)Village officer (b)Security guard (c)Health attendant (d)Police man (e)A farmer [ ]
2. Why was the whole village flooded? ____ (a)Because it is in the valley. (b)Because it is in the highlands. (c)Because it is in the desert. (d)Because it is near the valley. (e)Because it is near the highlands. [ ]
3. What did Nusura and her mother do to get out of their house? _____________ (a)Pulling the door. (b)Having fear. (c)Running together. (d)Crying together. (e)Moving to Nusura‟s aunt. [ ]
4. Why was the place where Nusura‟s aunt lives not flooded? ___________ (a)It did not rain at that place. (b)Her house had enough trenches. (c)It is in the highlands. (d)Her house was surrounded with a wall fence. (e)Her house had a strong roof. [ ]
5. What do you learn from the story that you have listened to? ________ (a)Building in the highlands is dangerous. (b)We should not stay with our mother only. (c)We should buy a house when floods occur. (d)Living in the valleys is dangerous. (e)Parents should not do evening work. [ ]

6. Our teachers always ______ us on having a personal time table. (a)reminds (b)remind (c)is reminding (d)reminding (e)has reminded [ ]
7. Masikilizano is a disciplined pupil. He easily breaks friendship with pupils who misbehave. In short, he does not _ bad behaviours. (a)toleration (b)tolerates (c)tolerate (d)tolerated (e)tolerating [ ]
8. Chapakazi and Chaupole ____________________ their home work before going to bed. (a)completed (b)completing (c)completely (d)complete (e)completes [ ]
9. Mainda bought a new English grammar book. The book ____________________________ in 2018. (a)has published (b)was published (c)had published (d)be published (e)have published [ ]
10. Last week Kamila received a letter from her mother. This week Kamila ___ a letter to her mother. (a)write (b)writing (c)wrote (d)writes (e)written [ ]
11. These cars belong to my brother. They are ________ (a)his (b)he (c)him (d)he‟s (e)hers [ ]
12. This is my note book. Where is _________? (a)your (b)yours (c)you are (d)yours‟ (e)your‟s [ ]
13. Most of the pupils prefer eating rice __________ ugali. (a)to (b)than (c)too (d)with (e)and [ ]
14. We went _________ along Mkuyuni road. (a)straight (b)left (c)right (d)backward (e)centre [ ]
15. Mwajuma is coming back __________the library with an English language book. (a)to (b)in (c)from (d)through (e)off [ ]
16. The furious snake escaped __________ the basket. (a)from (b)onto (c)in (d)inside (e)off [ ]
17. Do you sell ____________ sugar in your shop? (a)many (b)any (c)few (d)some (e)much [ ]
18. Happy was asked that, “Do you play netball?” How would she answer the question in a positive contracted form? ___________________________ (a)Yes, I did. (b)Yes, she plays. (c)Yes, I do. (d)Yes, we do. (e)Yes, she does. [ ]
19. The boy said, “I am a good boy.” How would you report what he said indirectly? _________________ (a)The boy said that he was a good boy. (b)The boy said that he is a good boy. (c)The boy saidthat I am a good boy. (d)The boy said that had been a good boy. (e)The boy said that he has been a good boy. [ ]
20. “Teachers teach pupils.” How would this sentence read in a passive form? ______________________ (a)Pupils are teaching teachers. (b)Pupils teach teachers. (c)Pupils are taught by teachers. (d)Pupils are being taught by teachers. (e)Pupils were being taught by teachers. [ ]
21. Suppose that the day after tomorrow will be Saturday, what day will tomorrow be? ____________ (a)Sunday (b)Wednesday (c)Thursday (d)Friday (e)Tuesday [ ]
22. The shepherd blocked a number of ___________ from entering Mr.Maguru's farm. (a)ships (b)ship (c)sheeps (d)sheep (e)sheep‟s [ ]
23. Mrs.Chapakazi told her pupils, “Rewrite your names at the back of your exercise books”. The underlined word means to _______________ (a)correct (b)bold (c)erase (d)repeat (e)clarify [ ]
24. Daudi‟s father is a medical doctor. He therefore ____ sick people. (a)treats (b)welcomes (c)warns (d)cares for (e)checks [ ]
25. The waitress was very slowin serving the guests. What is the opposite of the underlined word in the sentence? _________________________________ (a)fast (b)weak (c)active (d)happy (e)lazy [ ]
26. I came to realise that the teacher was right but the pupils ____________ the question. (a)misunderstand (b)understood (c)understand (d)misunderstood (e)misunderstands [ ]
27. A fishmonger ___________________________ fish. (a)sells (b)eats (c)cooks (d)boils (e)dries [ ]
28. The pupils are advised to be ___________________ when they are being taught in a class. (a)attending (b)attention (c)attentive (d)attended (e)attendant [ ]
29. Peter and Salum are in form two at a boys‟ secondary school in Kwimba districtand they have the top leader intheir students‟ government. How is this leader called? ________________ (a)the head

leader (b)the head girl (c)the school prefect (d)the prefect chairperson (e)the head boy [ ]

30. The oppositeof the underlined word in the sentence, They arrived from Tanga at 8.00 am" is __________. (a)left (b)took-off (c)departed (d)flew (e)gone [ ]
31. Mr.Nguvumali likes the environment. He is in the garden ___________ flowers. (a)watering (a)pouring (c)raining (d)drying (e)draining [ ]
32. Upendo is joyful. The word "joyful" means ___________________. (a)happy (b)sad (c)angry (d)awkward (e)wonderful [ ]
33. The weather in Africa is generally hot. Europe experiences the opposite. It is mostly ___ over there. (a)warm (b)cold (c)hot (d)hotter (e)wet [ ]
34. Mr.Kavishe has a big farm of trees. Most of the trees in the farm have already shed their _____________. (a)leaf (b)branch (c)leaves (d)stem (e)branches [ ]
35. Plumbers often _______ our taps once in six months. (a)fixing (b)fixes (c)fix (d)fixed (e)fixs [ ]

**SECTION B: ARRANGE THE SENTENCES SO AS TO MAKE A GOOD COMPOSITION BY GIVING THEM LETTERS A – E.**

36. I hope we shall meet during the December holiday at home. [ ]
37. I wish you the best in your exams. [ ]
38. Dear Kajala. [ ]
39. I heard that you will write your annual examinations in December, 2021. [ ]
40. Thank you for your letter. [ ]

**SECTION C: READ THE FOLLOWING PASSAGE CAREFULLY AND ANSWER THE QUESTIONS THAT FOLLOW BY WRITING THE CORRECT ANSWERS**

*My name is Mwema, a pupil at Tunaweza girls' primary school. Last month I visited my grandmother at thevillage called Chevuko. Our bus left Mwendapole bus stand at 7:00 a.m. We arrived at Chevukobus stand eleven hours later. My uncle's children Zuraya and Rosta came to pick me up fromthe bus stop and took me home.*

*Although it was a very long journey, I enjoyed seeing wild animals on the way. I saw animals such as Lions, Impalas, Zebras and Giraffes. I was veryexcited to seea Lion beside the road. My grandmother was very happy to see me because we had notmet for a long time.*

*During the whole timeat my grandmother"s place, I enjoyed looking after the animals she keeps. She keeps cows, goats and sheep. I also enjoyed listening to the stories she used to tell us in the evening about her lovely village.*

**QUESTIONS**

41. How the village Mwema visited is called? ________________________________________
42. Imagine you were sibling to Rosta and Zuraya. How would you call Mwema? ____________________
43. What is the collective name for the animals kept at home by Mwema"s grandmother? _____________
44. Why was Mwema"sgrandmother happy? ______________________________________
45. Why did Mwema enjoy the journey though it was verylong? _______________________________

# PASSAGE

*My name is Nusura. I live in Mabondeni village. A large part of our village is in the valley. Two years ago, it started raining with light showers. No one knew what was about to happen. A few hours later, it started raining heavily. Water was all over our house. My mother came and woke me up.*

*Neither my mother nor I had any idea on what to do. That day my father was not at home. He had gone for the evening shift as he is a security guard at Jambo hospital.*

*I saw fear in my mother's eyes. I stood firmly and joined her in pulling the door. Finally we opened it. We moved to my aunt who lives in the highlands. At my aunt's place there were no floods although it was also raining there. When we were at the hills we saw the whole village flooded. My aunt was not only happy to see us but also took pity on us. When my father got the news about the floods, he immediately came to my aunt's place. He promised to rent a house in the highlands. We now no longer live in the valley.*

# MARKING SCHEME

## ENGLISH LANGUAGE – STANDARD VII

| No | Answer | No | Answer | No | Answer |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | 21 | | 41 | |
| 2 | | 22 | | | |
| 3 | | 23 | | | |
| 4 | | 24 | | | |
| 5 | | 25 | | 42 | |
| 6 | | 26 | | | |
| 7 | | 27 | | | |
| 8 | | 28 | | | |
| 9 | | 29 | | 43 | |
| 10 | | 30 | | | |
| 11 | | 31 | | | |
| 12 | | 32 | | | |
| 13 | | 33 | | 44 | |
| 14 | | 34 | | | |
| 15 | | 35 | | | |
| 16 | | 36 | | | |
| 17 | | 37 | | 45 | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 18 | | 38 | | | |
| 19 | | 39 | | | |
| 20 | | 40 | | | |

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA

## SHULE YA MSINGI RWENSINGA

## JARIBIO LA SOMO MAARIFA YA JAMII DARASA LA VII JUMATATU 20.01.2022

**CHAGUA HERUFI YA JIBU SAHIHI**

1. **Ardhi ni rasilimali ambayo isipotunzwa vizuri inaweza kusababisha hatari katika maisha ya viumbe hai na rasilimali nyingine. Ipi ni njia bora itakayotumika kutunza rasilimali hiyo kati ya zifuatazo? ______ (a)Kuongeza idadi ya wakulima mashambani (b)Kutoa elimu juu ya matumizi sahihi yaardhi (c)Kuhimiza wafugaji kuongeza idadi ya mifugo (d)Kuwahimiza wananchi kutumia mbolea za viwandani (e)Kuhimiza upandaji miti katika maeneo ya wazi [ ]**
2. **Katika sikukuu ya wakulima kauli mbiu iliyotolewa na Waziri Mkuu ilikuwa ni, "Kilimo ni uti wa mgongo katika uchumi wa Tanzania". Kauli mbiu hiyo inamaana gani? ____________________________ (a)Ni shughuli inayofanywa na watu matajiri (b)Hufanyika kwa kutumia matrekta na majembe ya kukokotwa na ng'ombe (c)Ndio shughuli kuu ya uzalishaji mali (d)Hufanyika sehemu zenye vyanzo vya maji pekee (e)Mazao yanayovunwa huuzwa nje ya nchi [ ]**
3. **Mwalimu Kazimoto alifundisha kuhusu shughuli ya kilimo cha mazao ya biashara kilichofanywa Tanganyika kabla ya uhuru. Je, wanafunziwalibaini mazao yapi ya biashara? _____________________ (a)Korosho, maharage,mkonge na pareto (b)Mahindi, kahawa, chai na pareto (c)Kahawa,pareto,mkonge na chai (d)Zabibu, kahawa,chai na maharage (e)Pareto, korosho,chai na mahindi [ ]**
4. **Wakulima wengi nchini Tanzania hupeleka mazao sokoni kuuza. Ninjia zipi kuu za usafirishaji zinazotumika? _________________________ (a)Barabara na Reli (b)Anga na Barabara (c)Maji na Anga (d)Reli na Anga (e)Maji na Barabara [ ]**
5. **Shughuli za kilimo huweza kuharibu ardhiikiwa hazikufanyika kwa uangalifu. Ni kwa namna gani kilimo kinaweza kuharibu ardhi? ______ (a)Kwa kutumia mbolea ya asili (b)Kwa kulima kwa kubadilisha mazao (c)Kwa kulima matuta ya kukinga mteremko (d)Kwa kutumia mbolea za viwandani (e)Kwa kupanda miti karibu na shamba [ ]**
6. **Ukurasa wa 3kati ya 96.Shamba la Bwana Tembo ambalo lipo pembeni ya mlima Pina limepungukiwa na rutuba kutokana na momonyoko wa udongo. Kama mtaalam wa mazingira ninini chanzocha momonyoko huo? ________________________________ (a)Shamba kuwa katika mteremko mkali (b)Shamba kuwa na miti mingi (c)Samadi kuwekwa shambani (d)Shamba kupandwa mazao mengi ya mizizi na nafaka (e)Mazao kubadilishwa shambani kila mwaka [ ]**
7. **Shughuli za kibinadamu kandoya mto Matumaini huleta madhara kwa jamii inayouzunguka. Ni madhara gani yanasababishwa na shughuli za ukataji miti ovyo pembeni mwa mto huo? _________ (a)Ukosefu wa maji viwandani (b)Uchafuzi wa hewa (c)Ardhi kupoteza rutuba (d)Kukauka kwa vyanzo vya maji (e)Kupungua kwa uvuvi [ ]**
8. **Wazo ni mkulima ambaye anataka kuanzisha kilimo katika eneo ambalo ni nusu jangwa. Kama Afisa kilimo niushauri gani utampa?________ (a)Kulima mazao yanayovumilia ukame (b)Kuachana na shughuli za kilimo (c)Kulima msimu wa mvua tu (d)Kutumia mbolea ya viwandani tuwakati wa kilimo (e)Kutumia samadi peke yakewakati wa kilimo [ ]**
9. **Ukiwa ni kiongozi wa klabu ya kutunza mazingira, utampa ushauri gani mtu anaye kata miti ovyo kwa ajili ya kupata nishati? ___________________ (a)Kutumianishati mbadala rafiki kwa mazingira (b)Kujificha asikamatwe na Maafisa Misitu (c)Kuhifadhivyema mabaki ya miti iliyokatwa (d)Kuuzakuni na mkaa kujiongezea kipato (e)Kukatamiti ya ndani ya misitu ili asijulikane [ ]**
10. **Ni tukio lipi la kihistoria lilitokea Tanganyika mwaka 1926? _______ (a)Kuanza kwa Vita Kuu ya Pili ya Dunia (b)Kuanzishwa kwa chama cha African Association (c)Kuanzishwa kwa Baraza la Bunge (d)Uhuru wa Tanganyika (e)Kuanzishwa kwa vyama vingi [ ]**
11. **Ukurasa wa 4kati ya 911.Wanafunzi wa Darasa la Saba katika Shule ya Msingi Mwenge wanapanga safari ya kimasomokwenda kuona mabaki yamifumo ya kilimo cha umwagiliaji iliyotumiwa na watu wa kale. Ni eneolipi la kihistoria utawashauri kutembelea? _________ (a)Engaruka (b)AmboniClsimila (d)Olduvai Gorge (e)Kondoa Irangi [ ]**
12. **Maeneo yafuatayo ya kihistoria yanapatikana Tanzania isipokuwa _________________________________ (a)Rusinga (b)Olduvai Gorge (c)Engaruka (d)Kondoa Irangi (e) Kaole [ ]**
13. **Historia ya ukombozi wa Tanzania ilianza na vyama vya ustawi wa wafanyakazi kama vile TTACSA mwaka 1922 kilichobadilishwa kuwa TAA mwaka 1929 na baadae kuwa TANU mwaka 1954. Je, ni kwa nini TAA ilibadilishwa kuwa chama cha TANU mwaka 1954? ____________ (a)Kuwaunganisha watu wote katika kudai uhuru (b)Kuwa chama cha kisiasa kwa ajili ya wafanyakazi tu (c)Kuwaunganisha watu wote kupigana vita vya ukombozi (d)Kuunganisha vyama vyote vya siasa katika harakati za ukombozi (e)Kuwa chama cha kutetea ustawi wa wakulima [ ]**

14. Wanafunzi wa Darasa la Sita walirekodi viwango vya jotoridi kuanzia Jumatatu hadi Jumapilikama ifuatavyo:200C, 320C, 300C, 240C, 270C, 270C na 220C mtawalia. Je,upi ni wastani wa jotoridi kwa wiki? __________ (a)200C (b)320C (b)270 (d)26.20C (e)260 [ ]
15. Umepewa jukumu la kutoa mafunzo kwa wanakijiji wa Kijiji cha Juhudi juu ya fursa mbalimbali za kibiashara ambazo zinaweza kufanyika katika vipindi mbalimbali vya mwaka. Je, ungewashauri kufanya biashara ya kuuza miavuli katikakipindi gani? ________________ (a)Wakati wa Kiangazi (b)Wakatiwa Kipupwe (c)Wakati wa Vuli (d)Wakati wa Masika (e)Wakati wa Baridi [ ]
16. Wanafunzi wa Darasa la Nne walifundishwa kuhusu vipengele mbalimbalivya hali ya hewa. Ni kundi lipilinawakilisha vipengele vya hali ya hewa walivyojifunza? ________________________________ (a)Jotoridi, udongo, mvua na unyevuanga (b)Anga, mwangajua, mgandamizohewa na upepo (c)Maji, udongo, jotoridi na mawingu (d)Mgandamizohewa, jotoridi, mvua na mwangajua (e)Mvua, jotoridi mgandamizohewa na anga [ ]
17. Baraka anatafuta msaada wako kumwezesha kujibu swali kuhusu dhana ya "utamaduni". Je, ni vielelezo vipi vya utamaduni utakavyo-mpa Baraka ili aweze kuielewa vizuri dhana hiyo? ________ (a)Lugha, mila na tohara (b)Mila, desturi na lugha (c)Mila, desturi na miiko (d)Tohara, mila na desturi (e)Lugha, mila na makumbusho [ ]
18. Ngoma za asili, uchongaji, uchoraji na maigizo ya jadi ni miongoni mwa mambo ya kitamaduni yanayovutia watalii. Ni neno gani lifaalo kwa vipengele hivi vya utamaduni? ________________________ (a)Mila (b)Sanaa (c)Michezo (d)Lugha (e)Miiko [ ]
19. Kiongozi kutoka Wizara inayosimamia Utamaduni aliwataka vijana kuacha kushabikia tamaduni za kigeni na kudharau tamaduni za Kiafrika. Je, nini lengo la ushauri huo? ________________________ (a)Kulinda maslahi ya wageni (b)Kulinda maslahi ya viongozi (c)Kupata fursa ya kutembelea nchi za nje (d)Kulinda rasilimali za Taifa (e)Kufurahiarasilimali za Taifa [ ]
20. Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Harambee husisitiza wanafunzi wake kushiriki katika michezo ya jadi. Lipi katiya yafuatayo ni lengo lake kuu? ________________________ (a)kukuza kufikiri na kucheza (b)kuwezesha maamuzi na kuwa mbinafsi (c)kukuza kufikiri na kufanya maamuzi (d)kuongeza uzuri wa nyimbo na kufikiri (e)kutanua utawala wa sheria nakufanyamaamuzi [ ]
21. Fikiria umeteuliwa kuongea na mojawapo ya makundi rika katika jamii yako kuhusu mahusioano mema miongoni mwao. Lipi kati ya yafuatayo ungelisisitiza? ________ (a)Kuheshimiana na kusaidiana (b)Kusaidiana na kugombana (c)Kusalimiana na kudharauliana (d)Kuheshimiana na kubaguana (e)Kuelewana na kuogopana [ ]
22. Kama kuna wazazi na watoto, hii ni familia ya awali. Je, familia hii itaitwaje baada ya vifo vya wazazi wao? ______________________ (a)Familia pana (b)Familia ya watoto (c)Familia ya watoto yatima (d)Familia tegemezi (e)Familia ya watoto wa mitaani [ ]
23. Ukoloni katika nchi nyingi za Kiafrika ulikuwa na hasara zaidi kuliko faida. Kama mwanahistoria, ipi unadhani ni athari ya kijamii iliyotokana naukoloni katika Tanganyika? ______________________ (a)Kusaini mikataba na watawala wenyeji na kuleta mazao mapya (b)Kuanzishwa kwaelimu rasmi na kueneza Ukristo (c)Kusaini mikataba na watawala wenyeji na kujenga barabara (d)Kuanzishwa kwa mazao mapya na kuteua machifu kama watawala (e)Kuleta elimu rasmi na kusaini mikataba na watawala wenyeji [ ]
24. Nchi nyingi za Afrika kuwa wanachama wa jumuiya mbalimbali inadhihirisha umuhimu wa jumuiya hizokwa nchi husika. Unadhani nini kitatokea endapo nchi itavunja uhusiano huo? ________ (a)Kutakuwa na maendeleo makubwa katika nchi (b)Kushuka kwa uchumi na kudorora kwa amani (c)Kutumia bidhaa za nchi nyingine na kukua kwa maendeleo (d)Kuongeza wajuzi katika nchi na dunia (e)Kupata fursa ya kuungana na mataifa tajiri [ ]
25. Mnamo robo ya mwisho ya karne ya 19, Mataifa ya Ulaya yaligombea maeneo ya Afrika kwasababu walitaka malighafi, masoko, wafanyakazi na sehemu ya kuweka vitega uchumi. Maeneo yafuatayo yaligombaniwa isipokuwa __________________ (a)Maeneo ya kando kando ya Bahari au Ukanda wa Pwani (b)Maeneo yenye hali ya hewa nzuri na ardhi yenye rutuba (c)Maeneo yenye maziwa na mito mikuu (d)Maeneo yenye utajiri wa madini na rasilimali nyingine (e)Maeneo yenye viwanda vingi vya kuzalisha bidhaa [ ]
26. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere anatambulika kuwa ni shujaa hapa Tanzania na Afrika kwa ujumla. Ni nini kinachomfanya atambulike hivyo? ______________ (a)lihudhuria vikao vya UNO huko Ulaya (b)Alipinga vikali aina zote za ubaguzi wa rangi na kidini (c)Alipinga vikali urejeshwaji wa mfumowa vyama vingi (d)Aliwahamasisha Watanganyika kutumia mapambano ya silaha (e)Alihamasisha mapinduzi katika kupigania uhuru [ ]
27. Kuanzia mwaka 1985 hadi 2015 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliongozwa na marais watatu. Ipi ni orodha sahihi ya Marais hao? ________ (a)Julius K. Nyerere, Ali H. Mwinyi and Bejamin W. Mkapa (b)Julius K. Nyerere, Ali H. Mwinyi na Jakaya M. Kikwete (c)Ali H. Mwinyi, Benjamin W. Mkapa na Jakaya M. Kikwete (d)Julius K. Nyerere, Abeid A. Karume na John P. Magufuli (e)Benjamin W. Mkapa, Jakaya M. Kikwete na John P. Magufuli [ ]
28. Mwalimu aliwaambia wanafunziwakekuwa mistari ya latitudo huwa na mizingo tofauti tofauti kutegemea na mahali ulipo. Ni mstari upi wenye mzingo mrefu kati ya hii ifuatayo?______________________________ (a)Tropiki ya Kaprikoni (b)Mzingo wa Aktiki (c)Mstari wa Ikweta (d)Tropiki ya Kansa (e)Mzingo wa Antaktiki [ ]
29. Wakati wa kipindi cha somo la Maarifa ya Jamii mwalimu aliwapa wanafunzi ramani ya Tanzania yenye vitu vya asili na vilivyotengenezwa na binadamu kwa lengo la kujifunza. Je, hiyo ilikuwa ni ramani ya ainagani? ______________________________ (a)Ramani za takwimu (b)Ramani za kisiasa (c)Ramani za kontua (d)Ramani za topografia (e)Ramani za miji [ ]
30. Mtalii aliwasili nchini Tanzania kupitia uwanja wa ndege wa Kilimanjaro na kuelekea moja kwa moja katika hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro bila ya kupokelewa na mwenyeji yeyote. Ni kifaa kipikati ya vifuatavyo kilimwezesha kufika huko? ______________ (a)Skeli (b)Hali ya hewa (c)Ramani (d)Mwelekeo wa jua (e)Picha 3 [ ]
31. Bahati alichora ramani ya kijiji chao bila kuonesha kipimio cha ramani. Ni adhari ipi atakayoipata mtumiaji wa ramani hiyo? ______________________ (a)Kushindwa kufahamu mipaka ya kijiji (b)Kutofahamu ukubwa halisi wa kijiji (c)Kutozitambua alama zilizotumika (d)Maudhui ya ramani kutoeleweka (e)Mazao ya chakula yaliyo kijijini kutoonekana vizuri [ ]
32. Fikiria kuwa umealikwa kamamtaalamu wa mambo ya hali ya hewakuelezea umuhimu wa tabaka la ozoni kwajamii. Je,ungeelezanini? ______________________________________ (a)Huzuia kansa ya ngozi (b)Huzuia mmomonyoko wa udongo (c)Huongeza idadi ya watu (d)Husababisha kutengenezeka kwa mvua (e)Huongeza uoto wa asili [ ]
33. Rafiki yangu alisafiri kwenda Ulaya kumtembelea shangazi yake kipindi cha likizo. Kulikuwa na baridi kali iliyoambatana na mchana kuwa mfupi kuliko usiku. Je, hali hiyo inawakilisha msimu upi wa mwaka? ____________________________________________ (a)Kiangazi (b)Masika (c)Kipupwe (d)Vuli (e)Mvua [ ]
34. Wanafunzi wa Darasa la Tatu walijifunza kuwa,kuna sayari nane zinazounda mfumo wa jua ambazo baadhi zipo mbali na nyingine zipo

karibu na jua. Je, ni Sayari ipi miongoni mwa zifuatazo ipo karibu zaidi na jua? ____________________
(a)Sumbula (b)Kausi (c)Zuhura (d)Zebaki (e)Dunia [ ]

35. Tanzania ni nchi iliyojaaliwa kuwa na madini ya aina mbalimbali. Ni kundi lipi kati ya yafuatayo hujumuisha madini ya vito? ________
(a)Dhahabu, chumvi na chuma (b)Almasi, rubi na tanzanaiti (c)Almasi, dhahabu na chuma (d)Cobalt, rubi na tanzanaiti (e)Chumvi, dhahabu na almasi [ ]

36. Wanafunzi wa Darasa la Saba walipewa aina mpya ya vifungo kwa ajili ya mashati yao. Ni kanuni ipi wanapaswa kuzingatia wakati wakushona vifungo hivyo? ____________________
(a)Kuchagua uzi wenye rangi tofauti na vifungo walivyopewa (b)Kuchagua sindano inayoendana na kitambaa cha shati (c)Kuanza kushona mshono wa kushikiza (d)Kutumia sindano kubwa kuliko tundu la kifungo (e)Kupitisha uzi upande wa juu ya kitambaa cha shati [ ]

37. Umemtembelea shangazi yako na kupewa chumba kichafu cha kulala. Ni magonjwa gani unaweza kuyapata kwa kulala kwenye chumba hicho? ____________________
(a)Kuharisha na kutapika (b)Kukohoa na kutapika (c)Mafua na kifua (d)Malaria na kifua (e)Kuharisha na mafua [ ]

38. Bwana Nzima amepanga kusafiri na amedhamiria kufungasha nyama kwa ajili ya safari yake. Ungemshauri kutumia mojawapo ya njia zipi kuandaa nyama hiyo ili kuzuia kuharibika? ____________
(a)Kukaanga, kuchemsha na kuchoma (b)Kuchemsha, kubanika na kukaanga (c)Kutokosa, kukaanga na kuchoma (d)Kuchoma, kukaanga na kubanika (e)Kuchoma, kubanika na kupika kwa mvuke [ ]

39. Mwalimu wa Stadi za Kazi aliwaongoza wanafunzi kufinyanga chungu na kuwapa mbinu za kukikausha vizuri. Je, kuna umuhimu gani wa kukikausha chungu hicho? ____________________
(a)Kukifanya kiwe imara (b)Kukifanya kiwe na rangi nyeusi (c)Ili kuweza kukiweka nakshi (d)Kukifanya kuwana harufu ya kuungua (e)Kukifanya kiwe chepesi [ ]

40. Mimi ni mbunifu, mwenye uthubutu na ninajituma katika kutimiza malengo yangu. Je, mimi ni nani? ____________________
(a)Mjasiriamali (b)Mtu mwenye ujuzi (c)Mfanyabiashara (d)Mnunuzi (e)Muuzaji [ ]

**SEHEMU B**

**JIBU MASWALI YAFUATAYO KWA KUELEZA KWA KIFUPI**

41. Eleza kwa kifupi tofauti kati ya mjasiriamali mtumishi na mjasiriamali mfanyabiashara? ____________________
____________________
____________________

42. Mlipuko wa volkano katika kijiji cha Kikuu umeleta madhara kwa jamii. Bainisha madhara chanya mawili ya mlipuko huo
____________________
____________________
____________________

43. Bi Atupele aliwataka wanafunzi waorodheshe tabia ya nchi ya maeneo waliyotoka. Mmoja wa wanafunzi alitaja kuwepo kwa mvua nyingi, kiwango cha juu cha jotoridi na uwiano mdogo wa joto kwa mwaka mzima. Je, eneo hilo lina tabia gani ya nchi?
____________________
____________________
____________________

44. Tabu alitembelea kituo cha hali ya hewa kilichopo uwanja wa ndege wa Mwanza kuchukua takwimu za hali ya hewa ya eneo hilo, na kuwasilisha takwimu hizo katika Jedwali kama ifuatavyo:
(a) Ni mwezi upi ulikuwa na mvua na jotoridi kubwa?
____________________
____________________
(b) Ni aina ipi ya tabia ya nchi inawakilishwa na taarifa zilizopo kwenye jedwali? ____________________

45. Ni kwa nini Chifu Mkwawa alijulikana kama shujaa katika jamii yake
____________________
____________________
____________________

# MAJIBU YA JARIBIO

## SOMO LA MAARIFA YA JAMII – DARASA LA VII

| Na | Jibu | Na | Jibu | Na | Jibu |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | 21 | | 41 | |
| 2 | | 22 | | | |
| 3 | | 23 | | | |
| 4 | | 24 | | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 5 | | 25 | | 42 | |
| 6 | | 26 | | | |
| 7 | | 27 | | | |
| 8 | | 28 | | | |
| 9 | | 29 | | 43 | |
| 10 | | 30 | | | |
| 11 | | 31 | | | |
| 12 | | 32 | | | |
| 13 | | 33 | | 44 | |
| 14 | | 34 | | | |
| 15 | | 35 | | | |
| 16 | | 36 | | | |
| 17 | | 37 | | 45 | |
| 18 | | 38 | | | |
| 19 | | 39 | | | |
| 20 | | 40 | | | |

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA

## SHULE YA MSINGI RWENSINGA

## JARIBIO LA SOMO URAIA NA MAADILI DARASA LA VII JUMATATU 20.01.2022

**SEHEMU A**

1. **Ni jambo zuri kuamka asubuhi na mapema na kufanya mazoezi ya viungo. Je, mazoezi ya viungo yanaweza kukusaidia nini? ____________ (a)Kuwa mkakamavu na nadhifu (b)Kuwa mwenye afya na nguvu (c)Kutokwa jasho na kuhisi joto (d)Kutetemeka na kuhisi baridi (e)Kuwa dhaifu na mgonjwa [ ]**
2. **Jina la Tanzania lilianza kutumika baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Je, ni mwaka gani jina hilo lilianza kutumika? ____ (a)1962 (b)967 (c)1964 (d)1992 (e)1961 [ ]**
3. **Ngazi ya juu ya uongozi katika serikali ya kata ni cheo cha Diwani. Ni kwa namna gani kiongozi huyo hupatikana? _____ (a)Maamuzi ya Baraza la madiwani (b)Maoni ya wananchi ndani ya kata (c)Maoni ya viongozi wa Baraza la Kata (d)Kupigiwa kura na wananchi wa kata husika (e)Maamuzi ya serikali ya kata [ ]**

4. Je, ni mbinu ipi kati ya zifuatazo inaweza kutumika kuitangaza Shule yako? ______________________ (a)Ufaulu wa wanafunzi (b)Utajiri wa wanafunzi (c)Wingi wa wanafunzi (d)Uchangamfu wa wanafunzi (e)Usafi wa wanafunzi [ ]
5. Wanawake na wanaume wana wajibu na majukumu tofauti katika jamii. Ni neno gani linafafanua wajibu wa majukumu hayo? _____ (a)Stadi (b)Jinsia (c)Jinsi (d)Morali (e)Usawa [ ]
6. Kila raia wa Tanzania ana wajibu wa kulinda amani ya nchi yake. Onesha ni kwa vipi utatimiza wajibu huo? _______ (a)Kutii sheria za nchi (b)Kuwakaribisha wageni ndani (c)Kuwalinda wahamiaji (d)Kulinda katiba ya nchi (e)Kutumia vyombo vya dola [ ]
7. Ni muhimu kushiriki kuelimisha jamii kuhusu kutoa misaada kwa makundi maalum. Ni kwa namna gani unaweza kuhamasisha jamii kusaidia watu hawa? ____________________________ (a)Kuomba msaada kutoka katika kundi la vijana (b)Kutoa taarifa kupitia vyombo vya habari (c)Kufanya majadiliano na vyama vya siasa (d)Kuomba kwa kutumia wanasheria (e)Kuomba misaada maalum na mikopo [ ]
8. Kama mtoto unayeishi katika nyumba yenye ukandamizaji wa kijinsia. Je, ni hatua gani inaweza kutumika katika kutokomeza ukandamizaji wa kijinsia katika jamii?___(a)Kutoa elimu kwa wote (b)Kutoa elimu kwa wanaume (c)Kutoa elimu kwa watu wazima (d)Kutoa elimu kwa watoto (e)Kutoa elimu kwa vijana [ ]
9. Kwa kuzingatia uelewa wako kuhusu aina za familia, seti zifuatazo zinaonesha familia TANDAA isipokuwa ______________ (a)Mama, watoto na bibi (b)Baba, shangazi na mjomba (c)Shangazi, mjomba na watoto (d)Baba, mama na watoto (e)Babu, shangazi na mama [ ]
10. Kitendo cha mtoto wa kike kumsimulia Baba yake jinsi anavyoepuka kushawishiwa kufanya ngono na kijana wa kiume kinaitwa ________________________ (a)kujijali (b)uaminifu (c)uwazi (d)nidhamu binafsi (e)ustahimilivu [ ]
11. Mahusiano mabaya baina ya wanajamii yanaleta matokeo hasi katika jamii zetu. Nini athari ya kunyanyapaa? ___ (a)Kukosekana kwa amani na usalama (b)Kuimarika kwa upendo na urafiki (c)Kuongezeka kwa umaskini na ujinga (d)Kuongezeka kwa migogoro na mapigano (e)Kukuza urafiki na uvumilivu [ ]
12. Iwapo mwanafunzi mwenzako anaona woga kukemea vitendo visivyofaa vinavyofanyika shuleni kwake, utamshauri kutumia njia gani kufikisha maoni yake kwa uongozi? _______ (a)Kutumia sanduku la maoni (b)Kutumia mkutano wa wazazi kuelezea (c)Kumtuma mzazi wake kuelezea (d)Kumtuma mwalimu wake wa darasa kuelezea (e)Kutumia sanduku la posta [ ]
13. Mkuu wa Shule ya Msingi Sabasaba ameanzisha kitengo cha ushauri nasaha katika shule yake. Nini umuhimu wa kitengo hicho? ____ (a)Kutoa mwongozo wa jinsi ya kutatua changamoto (b)Kueleza matatizo ya wanafunzi hadharani (c)Kuwashauri wanafunzi wenye matatizo kujieleza (d)Kuwatangaza wanafunzi wenye matatizo (e)Kuwatenga wanafunzi wenye matatizo[ ]
14. Kundi lipi kati ya yafuatayo linaunda rasimali za Taifa? _________ (a)Misitu, magari na madini (b)Meli, ndege na ardhi (c)Pamba, karafuu na ardhi (d)Mito, bahari na meli (e)Madini, ardhi na mbuga za wanyama [ ]
15. Unatakiwa kuwaelimisha wanafunzi wenzako kuhusu tabia hatarishi. Je, ni tabia ipi hatarishi wanawake wanatakiwa kuepuka? __________________ (a)Kutembea mtaani nyakati za usiku (b)Kusoma nyakati za usiku na mtu wa jinsi tofauti (c)Kuwa na marafiki wa jinsi tofauti (d)Kuwa karibu na wazazi na watu wazima (e)Kutazama picha za wanyama pori [ ]
16. Riziki alielezwa umuhimu wa kushirikiana na wengine katika kutekeleza majukumu yake binafsi na ya shuleni. Ni majukumu yapi anayotakiwa kuyatekeleza? ___________________________ (a)Kufagia, michezo na kumwagilia bustani (b)Kumwagilia bustani, kudeki na kuwa kiongozi (c)Kufagia, kudeki na kumwagilia bustani (d)Kupiga kura, kufagia na kudeki (e)Kudeki, kusafisha zahanati ya kijiji na kufagia [ ]
17. Bwana Kadege ni Afisa Maendeleo wa Kijiji cha Mlimani ambaye huwaelimisha wanakijiji kuhusu majukumu ya kijamii. Ni jukumu lipi kati ya yafuatayo ni la kijamii? ________________________ (a)Kumwagilia bustani ya familia (b)Kufagia na kudeki nyumba (c)Kusafisha chumba cha kulala (d)Kushiriki katika ujenzi wa shule (e)Kulisha mifugo ya nyumbani [ ]
18. Rasimali za Taifa ni tunu zinazotakiwa kutunzwa na kuhifadhiwa. Nani ana wajibu wa kutunza na kuhifadhi rasilimali za Taifa? ________ (a)Maafisa wa polisi (b)Maafisa wa jeshi (c)Raia wote (d)Baba na mama (e)Viongozi wote wa serikali [ ]
19. Ni kwa nini wanafunzi na wasomi hufanya utafiti? _______ (a)Kupata majibu yatakayosaidia kutatua matatizo (b)Kujulikana na watu wengi katika jamii (c)Kuwajua watu vizuri katika maisha yao (d)Kuishi na watu kwa amani na usalama (e)Kuwaheshimu watu wote katika jamii [ ]
20. Kama mwanafunzi mwenye kujitolea katika kufanya kazi mbalimbali za shuleni na jamii, utatumia mbinu ipi kuwafanya wanafunzi wenzako wajitolee kama wewe? __________________ (a)Kuwashurutisha (b)Kuwatumikisha (c)Kuwahamasisha (d)Kuwafuatilia (e)Kuwaongoza [ ]
21. Juakali alitakiwa kuandaa kitabu kinachohusu mbinu za kupanga mipango ya maendeleo ya Shule. Unafikiri kitabu hicho kinatoa mwongozo kwa nani? __________________________________ (a)Mwalimu Mkuu (b)Mwalimu Mkuu Msaidizi (c)uongozi wa shule (d)Kamati ya shule (e)Baraza la Shule [ ]
22. Ni mbinu gani inaweza kutumiwa na Tanzania kuchochea maendeleo katika sekta mbalimbali? ______________________ (a)Kushiriki katika michezo (b)Kusafiri kwenda nje ya nchi (c)Kushiriki katika sherehe (d)Kufanya kazi kwa bidii (e)Kuwaheshimu watu wazima [ ]
23. Kayumba ni mwanafunzi aliye na tabia na uwezo wa kujiongoza na kutenda jambo kwa ufanisi bila kusimamiwa. Tabia hii ya Kayumba inaitwaje? ________________________________ (a)Wajibu binafsi (b)Uwajibikaji binafsi (c)Nidhamu binafsi (d)Mtazamo chanya (e)Upendo binadisi [ ]
24. Kujiwekea malengo katika maisha ni jambo la muhimu. Nini faida ya kujiwekea malengo? _______________________ (a)Kufahamu unatakiwa kufanya nini na wakati gani (b)Huwezesha kutumia muda mwingi kujisomea (c)Husaidia ujuzi kwa kuiga kutoka kwa wengine (d)Kupata ujuzi wa kutazamia katika mitihani (e)Kuwa tegemezi katika kufanya maamuzi shuleni [ ]
25. Kwa nini tunashauriwa kujifunza kutokana na makosa ya watu wengine? _________ (a)Hutusaidia kurudia makosa ya wengine (b)Hutuwezesha kuyatambua makosa yetu (c)Hutuwezesha tusirudie makosa ya wengine (d)Hutuwezesha kuandika makosa mbalimbali (e)Kutuwezesha kuiga makosa ya wengine [ ]
26. Katika jamii, watu hujifunza kutoka kwa wengine. Ni wanafunzi wa namna gani ambao ungependa kujifunza kutoka kwao? ______ (a)Wenye heshima kwa viongozi wa shule (b)Wanaopenda sana

neno la Mungu (c)Walio na bidii kufanya kazi za nyumbani (d)Walio na ujuzi wa kuongea lugha ya kiingereza (e)Walio na bidii kwenye masomo na nidhamu [ ]

27. Simbatano aliadhibiwa shuleni kwa utoro. Ni upi ushauri mzuri kwa Simbatano? ________ (a)Kutakiwa kukubali kosa na kurudia kosa hilo (b)Kujifunza kutokana na kosa hilo na kujirekebisha (c)Kukimbia kosa hilo na kulirudia baadaye (d)Kurudia kosa hilo na kuendelea kujifunza kwa makosa (e)Kukubali kosa hilo na kuendelea kujenga uaminifu kwenye jamii [ ]
28. Kuna umuhimu gani kwa wanafunzi kuuliza maswali wanapokuwa darasani? ________
(a)Kufundishana wakati wa kujifunza (b)Kutaka kujulikana (c)Kupata maarifa mapya na ujuzi (d)Kudumisha nidhamu ya darasa (e)Kuwafurahisha walimu darasani [ ]
29. Binadamu wote wamezaliwa huru na kuwa sawa katika utu na haki. Ni chombo gani kilipitisha na kutoa tamko la kimataifa la haki za binadamu? ________
(a)Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa (b)Mahakama Kuu ya Kimataifa (c)Baraza la Usalama la Kimataifa (d)Kamati Tendaji ya Kimataifa (e)Baraza la Udhamini la Kimataifa [ ]
30. Haki za binadamu nchini Tanzania zinalindwa na katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni kwa nini haki za binadamu ziliingizwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? ________ (a)Kuimarisha uwazi nchini (b)Kuongeza ufanisi katika utendaji (c)Kuongeza demokrasia na utu (d)Kuongeza maelewano nchini (e)Kuimarisha msingi wa uhuru, usawa na haki [ ]
31. Kutekeleza majukumu ya nyumbani ni muhimu kwa mwanafunzi. Ni jinsi gani mwanafunzi anaweza kuongeza ufanisi katika utendaji wa shughuli za nyumbani? ________ (a)Kutumia ratiba ya shule kutenda shughuli za nyumbani (b)Kufanya kazi kwa bidii shuleni na siyo nyumbani (c)Kutokwenda shule hadi akamilishe kazi zote za nyumbani (d)Kufanya tathmini ya utendaji wa majukumu yote ya nyumbani (e)Kutenda shughuli za nyumbani usiku mzima bila kulala [ ]
32. Unafiki katika jamii ni jambo lisilofaa kutokana na athari zake. Kipi kifanyike ili kuondoa unafiki katika jamii? ____ (a)Kutunga sheria kali dhidi ya unafiki (b)Kuunga mkono kwa nguvu wanafiki (c)Kueleza ukweli kuhusu unafiki (d)Kusikiliza na kupenda wanafiki wote (e)Kuwatenga wanafiki na watu wengine [ ]
33. Kila binadamu anayo haki ya kumiliki mali. Haki hii inapatikana katika kundi gani la haki za binadamu kati ya haya yafuatayo? _____ (a)Kiuchumi na kijamii (b)Kisiasa na kiuchumi (c)Kijamii na kiraia (d)Kiraia na kisiasa (e)Kiutamaduni na kiraia [ ]
34. Uhusiano mzuri katika jamii huchochea maendeleo. Mkakati gani uchukuliwe ili kuzuia tabia ya kuharibu uhusiano mzuri baina ya watu? ________
(a)Kuwaelimisha juu ya umuhimu wa mahusiano na umbea (b)Kuwaelimisha juu ya umuhimu wa uongo na umbea (c)Kujenga uelewa juu ya kuepuka wivu na kusengenya (d)Kujenga uelewa juu ya umuhimu wa kuwa huru na kusema uongo (e)Kujenga uelewa juu ya wajibu wa kuigiza na kusengenya [ ]
35. Ni hali ipi inatoa maana kamili ya neno AMANI? ________
(a)Hali ya kuwa huru, kupendwa na kuchukizwa (b)Hali ya utulivu, furaha na bila kuwa na hofu (c)Hali ya kuwa na furaha, huzuni na uwoga (d)Hali ya kuwa na furaha, uoga na mashaka (e)Hali ya kuwa na furaha, kukata tamaa na hasira [ ]
36. Kukua kwa utandawazi katika jamii yoyote huwa na manufaa na madhara yake. Nini madhara ya utandawazi katika jamii? ________
(a)Kuwepo kwa mmomonyoko wa maadili (b)Kudumaa kwa teknolojia ya habari (c)Kupungua kwa mwingiliano wa watu (d)Kupungua kwa fursa za ajira (e)Kudunishwa kwa huduma za kijamii [ ]
37. Jumuiya ya zamani ya Afrika Mashariki iliundwa kwa makubaliano ya viongozi wa nchi za Tanzania, Kenya na Uganda. Marais gani wa kwanza walihusika katika kuunda Jumuiya hiyo? ________ (a)Daniel A. Moi, Yoweri Museveni na Julius. K. Nyerere (b)Ally H. Mwinyi, Jomo Kenyatta na Yoweri Museveni (c)Milton Obotte, Daniel A. Moi na Ally H.Mwinyi (d)Ally H. Mwinyi, Yoweri Mseveni na Daniel A. Moi (e)Julius K. Nyerere, Milton Obotte na Jomo Kenyatta [ ]
38. Umoja wa Mataifa ni jumuiya iliyodhamiria kutekeleza malengo yake katika misingi ya amani na usalama. Misingi hii ilitumika kuandaa sera ya Tanzania ya uhusiano wa kimataifa. Ni jambo gani lilijumuishwa katika sera hiyo? ________
(a)Kukuza umoja wa makabila yetu nchini (b)Kuagiza silaha za kivita ili kulinda uhuru wetu (c)Kuongeza ubaguzi wa rangi (d)Kulinda uhuru na usalama wa nchi yetu (e)Kuhamishia ukoloni kwa mataifa mengine [ ]
39. Kwa nini ni muhimu kuanzisha na kudumisha uhusiano wa kimataifa? ________
(a)Kukuza elimu, biashara na michezo (b)Kuendeleza teknolojia, elimu na uuzaji silaha (c)Kuongeza biashara, teknolojia na vyanzo vya maji (d)Kuimarisha uuzaji silaha, michezo na elimu (e)Kukuza elimu, michezo na vyanzo vya maji [ ]
40. Mchangamano wa watu wenye asili tofauti bado unahitajika sana nchini Tanzania. Je, lipi kati ya yafuatayo linaeleza umuhimu wa kuishi na watu wenye asili tofauti hapa Tanzania? ________
(a)Kubadilishana ujuzi na uzoefu (b)Kujifunza tamaduni zingine (c)Kulinda uzalendo wetu (d)Kufahamu mipaka yetu (e)Kuondoa ubaguzi [ ]

**<u>SEHEMU B: JIBU KWA KUTOA MAELEZO KWA KIFUPI KATIKA MASWALI YAFUATAYO</u>**

41. Watu mbalimbali hujifunza kwa kushirikiana na kubadilishana maarifa na watu wengine katika jamii. Eleza faida mbili za kushirikiana na watu wengine katika kujifunza mambo mbalimbali
i. ________
ii. ________

42. Uaminifu na uwazi ni nguzo muhimu ili kupata maendeleo katika jamii. Eleza madhara mawili yanayotokana na kukosekana kwa uamifu na uwazi miongoni mwa wanafunzi
i. ________
ii. ________

43. Katika jamii zetu baadhi ya mila huathiri sana wanawake. Mojawapo ya mila hizi ni ukeketaji. Eleza madhara mawili yanayotokana na kitendo cha ukeketaji kwa wanawake
i. ________
ii. ________

44. Wahitimu wa Darasa la Saba waliosoma somo la Uraia na Maadili, wanawezaje kunufaisha jamii zao kwa elimu hiyo waliyoipata?
________
________

45. **Eleza mambo mawili yanayojenga utawala bora katika ngazi ya familia.**
i. ______
ii. ______

# MAJIBU YA JARIBIO

## SOMO LA URAIA NA MAADILI – DARASA LA VII

<table>
<tr><th>Na</th><th>Jibu</th><th>Na</th><th>Jibu</th><th>Na</th><th>Jibu</th></tr>
<tr><td>1</td><td>B</td><td>21</td><td>D</td><td rowspan="4">41</td><td rowspan="4"></td></tr>
<tr><td>2</td><td>C</td><td>22</td><td>D</td></tr>
<tr><td>3</td><td>D</td><td>23</td><td>B</td></tr>
<tr><td>4</td><td>A</td><td>24</td><td>A</td></tr>
<tr><td>5</td><td>B</td><td>25</td><td>B</td><td rowspan="8">42<br><br>43</td><td rowspan="8">i. Huweza kusababisha kifo<br>ii. Husababisha kutoka damu nyingi wakati wa kujifungua</td></tr>
<tr><td>6</td><td>A</td><td>26</td><td>E</td></tr>
<tr><td>7</td><td>E</td><td>27</td><td>B</td></tr>
<tr><td>8</td><td>A</td><td>28</td><td>C</td></tr>
<tr><td>9</td><td>B</td><td>29</td><td>A</td></tr>
<tr><td>10</td><td>A</td><td>30</td><td>E</td></tr>
<tr><td>11</td><td>A</td><td>31</td><td>D</td></tr>
<tr><td>12</td><td>A</td><td>32</td><td>A</td></tr>
<tr><td>13</td><td>A</td><td>33</td><td>A</td><td rowspan="4">44</td><td rowspan="4">i. Kuwa raia wema<br>ii. Kuishi kwa misingi ya ut<br>iii. uKutii sheria za nchi bila shuruti<br>iv. kuishi na jamii katika misingi ya maadili</td></tr>
<tr><td>14</td><td>E</td><td>34</td><td>C</td></tr>
<tr><td>15</td><td>A</td><td>35</td><td>B</td></tr>
<tr><td>16</td><td>C</td><td>36</td><td>A</td></tr>
</table>

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 17 | D | 37 | E | 45 | i. *Kila mwanafamilia kutimiza wajibu wake*<br>ii. *Wazazi kuwasikiliza watoto na kuwapatia haki zao za msingi*<br>iii. *Watoto kuwatii na kuwasaidia wazazi wao katika majukumu mbalimbali* |
| 18 | C | 38 | D | | |
| 19 | A | 39 | A | | |
| 20 | C | 40 | A | | |

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA

## SHULE YA MSINGI RWENSINGA

## JARIBIO LA SAYANSI NA TEKNOLOJIA DARASA VII JUMATATU 20.01.2022

**SEHEMU A**

1. **Ni katika kiungo kipi cha mfumo wa mmeng'enyo wa chakula virutubisho hufyonzwa? ______________________________ (a)Utumbo mwembamba (b)Utumbo mpana (c)Tumbo la chakula (d)Kifuko nyongo (e)Umio wa chakula [ ]**
2. **Kijiji cha Mirwa kilikumbwa na baa la njaa kutokana na uvamizi wa vipepeo. Je, vipepeo hao walikuwa katika hatua ipi ya ukuaji?_____ (a)Buu (b)Kipepeo. (c)Yai (d)Kiwavi (e)Tunutu**
3. **Ni kanuni ipi hutumika kuonyesha uhusiano uliopo kati ya mkondo wa umeme, volteji na ukinzani katika sakiti ya umeme?__ (a)RVI= (b)VRI= (c)VRI= (d)RIV= (e)VIR= [ ]**
4. **Katika gesi zifuatazo, ipi unaweza kuitumia kuzima kitu kinachowaka? ___________ (a)Oksijeni (b)Nitrojeni (c)Kabon monoksaidi (d)Hyadrojeni (e)Kaboni dayoksaidi [ ]**
5. **Umepewa kazi ya kutafuta densiti ya maji. Je utatoa jibu lako katika kizio gani? ________________________________ (a)Kg/m3 (b)J/sm3 (c)N/m3 (d)Kg/sm3 (e)m/sm36 [ ]**
6. **Umeambiwa ufungue Program jedwali, je ni hatua zipi utaufuata? ________ (a)Bofya menu ya start → Microsoft office →Programu jedwali (b)Bofya menu ya start → Microsoft word → Programu jedwali (c)Bofya menu ya start → program jedwali → Microsoft office (d)Bofya menu ya start → programu jedwali → Microsoft word (e)Bofya menu ya start → Microsoft office → Microsoft word [ ]**
7. **Kijana mwenye nguvu na afya alisukuma ukuta kwa muda wa dakika kumi na ukuta huo haukudondoka. Kwa nini kijana huyo anaonekana hajafanya kazi _____________ (a)Alisukuma ukuta ambao haukusogea umbali wowote (b)Alitumia nguvu kidogo katika kuusukuma ukuta huo (c)Hakufuata mbinu za kisayansi katika kuusukuma ukuta (d)Hakujua uzito wa ukuta aliokuwa anausukuma [ ]**
8. **Tabia ipi ya mwangahuwakilishwana upinde wa mvua unaoonekana katika mawingu ukiwana rangi mbalimbali saba? ___________________ (a)Kuakisiwa (b)Kusharabiwa (c)Kung'aa (d)Kutawanyika (e)Mnunuriko [ ]**
9. **Baadhi ya watuhutoaharufu mbaya mwilini licha ya kuwa wanaoga kila asubuhi na jioni. Je, ushauri upi unapaswa kutolewa kwaoili kuondokana na tatizo hilo? _______________ (a)Kutumia maji safi na salama (b)Kutumia maji safi na kupaka mafuta (c)Kusafisha sehemu za siri na kwapa (d)Kutumia sabuni na kupaka mafuta (e)Kutumia pafyumu [ ]**
10. **Madhara ya kuwa na VVU/UKIMWI yanaweza kuwa kwa mtu binafsi, familia au Taifa. Yafuatayo ni madhara kwa mtu binafsi isipokuwa ____________________________ (a)Hofu ya kifo (b)Kuugua mara kwa mara (c)Unyanyapaa (d)Kupunguza nguvukazi (e)Kupoteza diraya maisha [ ]**
11. **Ili kuzima moto katika kitu kinachowaka, inashauriwa kufunika kwa nguo nzito kama blanketi. Nini lengo la kufanya hivyo? ___________________ (a)Kuondoa gesi ya oksijeni (b)Kuondoa gesi ya kaboni dayoksaidi (c)Kuongeza gesi ya kaboni monoksaidi (d)Kuondoa gesi ya naitrojeni (e)Kupunguzanguvu ya moto [ ]**
12. **Nishati ya aina gani hupatikana kama matokeo ya vitu kugongwa na kupulizwa? ____________________________ (a)Nishati ya sauti (b)Nishati ya umeme (c)Nishati ya mwanga (d)Nishati ya mawimbi (e)Nishati ya joto [ ]**
13. **Ukitazama maji yaliyotulia vizuri utaiona sura yako. Kitendo hicho kinaonesha tabia gani ya mwanga? ________ (a)Kusafiri (b)Kupinda (c)Kupenya (d)Kuakisiwa (e)Kusharabiwa [ ]**
14. **Wanafunzi wa Darasa la Saba walifanya jaribio la kurusha juu kipande cha chuma na puto lililojazwa hewa. Matokeo yake puto lilielea juu na chuma kilianguka chini. Je ni sifa ipi iliwezesha puto kuelea? __________ (a)Kuwa na uzito na hewa kwa ndani (b)Kuwa na hewana uzito kwa ndani (c)Kuwa na uwazi na uzito kwa ndani (d)Kuwa na mabawa na hewa kwa ndani (e)Kuwa na uwazi nahewa kwa ndani [ ]**
15. **Namna ipi ya maada ni nyepesi zaidi kuliko zingine? _______ (a)Kimiminika (b)Barafu (c)Hewa (d)Maji (e)Yabisi [ ]**
16. **Mwalimu wa Darasa la Sita anataka kuandaa matokeo ya mtihani ya nusu muhula kwa kutumia programu ya tarakilishi ili kuokoa muda. Je,utashauri kutumia programu gani?**

_______ (a)Programu jedwali (b)Program andishi (c)Programu endeshi (d)Program tumizi (e)Programu sakuzi [ ]

17. Wanafunzi wa Darasa la Saba walipewa kazi ya kutengeneza antena. Je, ni hatua ipi ya kwanza wanatakiwa kuzingatia kabla ya kuanza kutengeneza antena? ___________________ (a)Kuchagua aina ya antenna (b)Kusanifu antenna (c)Kubaini matumizi ya antenna (d)Kuchagua vifaa vya kutumia (e)Kuunda antenna [ ]
18. Uwezo alimuona fundi mitambo akiweka kilainishi kwenye sehemu ya toroli inayoshikilia gurudumu. Je, nini umuhimu wa kufanya hivyo? _________________________________ (a)Kuzuia vumbi (b)Kufanya ziwe safi (c)Kuzuiakutu (d)Kuzuia uchafu (e)Kupunguza msuguano [ ]
19. Mwalimu mkuu amewapa Wanafunzi wa Darasa la saba kazi ya kupakia mifuko ya mahindi kwenye lori. Je,watatumia mashine ipi kurahisisha kazi hiyo? _____________________ (a)Kamba (b)Wenzo (c)Kabari (d)Gurudumu (e)Roda [ ]
20. Misumari yote iliyoachwa njena fundi seremala alipokuwa anarekebisha moja ya darasa la shule ilibadilika rangi na kuwa kahawia. Je, ninikilisababisha kutokea kwa rangi hiyo? _________________ (a)Unyevunyevu na oksijeni (b)Mwanga na oksijeni (c)Unyevunyevu na mwanga (d)Nitrojeni na unyevunyevu (e)Oksijeni na nitrojeni [ ]
21. Watoto walipotembelea hifadhi ya Taifa,walipewa kifaa kilichosaidia kuwaona wanyama waliokuwa mbali. Je, unafikiri walipewakifaa gani? ___________ (a)Hadubini (b)Periskopu (c)Darubini (d)Miwani (e)Kamera [ ]
22. Unahitaji kufanya nini ili kutoa msaada wa awali kwa mtu anayeungua moto uliosababishwa nakulipuka kwa mafuta ya petroli? __________ (a)Kumtoa nguo zote (b)Kummwagia maji (c)Kumfunika blanketi zito (d)Kumfunika na kitambaa cha baridi (e)Kumpeleka hospitali [ ]
23. Mkulima ameumwa na nyoka mguuni Kama mtaalamu wa sayansi, utampa msaada gani wa awali? _________________ (a)Kumpeleka hospitali (b)Kumfunga sehemu ya juu ya alipoumwa (c)Kumsugua kwa majivu na chumvi (d)Kumsafisha jeraha kwa maji safi na sabuni (e)Kumlaza chali huku miguu ikiwa juu [ ]
24. Ni jozi ipi inawakilisha magonjwa yanayotokana na kurithi kasoro katika vinasaba kutoka kizazi kimoja kwenda kingine? _____________ (a)Selimundu na hemophilia (b)Kifafa na homa ya ini (c)Ualibino na kichocho (d)Pumu na kaswende (e)Hemofilia na kifua kikuu [ ]
25. Umeshauriwa na vijana wenzako kujiunga na kikundi cha kufanya mazoezi. Kamamtaalamu katika sayansi ya afya, kwa nini ni muhimu kupokea ushauri huo? __________ (a)Kuimarisha uhusiano na watu (b)Kupata marafiki wema (c)Kuimarisha afya ya mwili (d)Kujua aina za michezo (e)Kujua wachezaji bora [ ]
26. Baada ya baba yao kupata homa kali, vidonda vya koo, kuvuja damu puani, masikioni na kinywani, watoto wake walionekana wakimkumbatia kama ishara ya upendo. Siku chache baadae, wote walipata dalili hizoza ugonjwa. Je waliugua ugonjwa gani? ______________________ (a)Ndui (b)Kichocho (c)Ebola (d)Kuhara damu (e)Kipindupindu [ ]
27. Asidi inayopatikana tumboni husaidia katika mmeng'enyo wabaadhi ya vyakula. Je, asidi hiyo ina kazi gani nyingine? ____________________________ (a)Kuwezasha ufyonzaji wa virutubisho (b)Kuua vijidudu ambavyo vipo kwenye chakula (c)Kuwezesha misuli ya tumbo kusaga chakula (d)Kuyeyusha madini ambayo yapo kwenye chakula (e)Kumalizia mchakato wa kumeng'enya chakula [ ]
28. Baada ya uchunguzi wa kitaalamu,iligundulika kuwa Bwana Chapakazi alikula chakula kilichokuwa na sumu. Ni ogani ipi ilitumika kupambana na matatizo ya afya aliyoyapata Bwana Chapakazi? __________________________________________ (a)Ini (b)Figo (c)Ngozi (d)Moyo (e)Mapafu [ ]
29. Ogani zipi zinaunda mfumo wa utoaji takamwili wa mamalia? ____ (a)Ini, figo, ngozi na mapafu (b)Figo, mapafu, nyongo na kongosho (c)Ini, figo, kibofu na mapafu (d)Ngozi, kibofu, figo na kongosho (e)Mapafu, ngozi, kibofu na figo [ ]
30. Mzee Karanga alijikata katika kidole chake,damu iliyokuwa ikitoka ilishindwa kuganda kwa muda mrefu. Je, unafikiri Mzee Karanga amekosa nini katika damu yake? ____________ (a)Seli nyekundu (b)Chembe sahani (c)Plazima (d)Seli nyeupe (e)Himoglobini [ ]
31. Mwalimu alifanya jaribio la kuotesha mbeguya mmea ndani ya kisanduku kilichokuwa na tundu upande mmoja. Baada ya kuota,ilipinda kuelekea upande wenye tundu. Je, matokeo hayo yanaonesha nini? _______________________________ (a)Mimea hukua kuelekea nje (b)Mimea hukua kufuata mwanga (c)Mimea huhitaji eneo la wazi ili ikue (d)Mimea hupinda wakati wa ukuaji (e)Mimea hujongea kwa kupinda [ ]
32. Ndugu yako ana matatizo ya kutoona mbali. Utamshauri atumie vyakula gani mara kwa mara ili vimsaidie katika tatizo lake? __________ (a)Ndizi, machungwa na karanga (b)Wali, nanasi na nyama (c)Embe, chungwa na spinachi (d)Karoti, mihogo na maharagwe (e)Mkate, ndizi na mihogo [ ]
33. Mwanafunzi anataka kutengeneza sakiti rahisi ili apate mwanga katika nyumba. Je, ni vifaa vipi anavyotakiwa kuunganisha ili kufikia lengo hilo _______ (a)Gropu, waya na swichi (b)Selikavu, fyuzi na kikata sakiti (c)Selikavu, waya na glopu (d)Swichi, ethi na fyuzi (e)Fyuzi, waya na ethi [ ]
34. Ungeambiwa utoe mfano wa kifaa chochote kinachotumika kama nyenzo daraja la pili,ungetaja kitu gani? __________ (a)Toroli (b)Mkasi (c)Nyundo (d)Koleo (e)Fagio [ ]
35. Ni kifaa kipi hutumika kuhifadhi kichakato kikuu? __________ (a)Monita (b)Skrini (c)Kashamfumo (d)Kibodi (e)Kiteuzi
36. Ipi ni kazi ya pau nyumbani kwenye programu andishi? _______ (a)Kufanya marekebisho kwenye waraka (b)Kuchomeka michoro kwenye waraka (c)Kuandaa yaliyomo kwenye waraka (d)Kuandaa barua pepe (e)Kuonyesha jina la faili [ ]
37. Sakiti ya umeme imeunganishwa na kikinza ambacho hakibadiliki. Nini kitatokea kwenye mkondo wa umeme ikiwa volteji itaongezeka? ___________________________________ (a)Mkondo wa umeme utaongezeka (b)Mkondo wa umeme hautobadilika (c)Mkondo wa umeme utapungua (d)Mkondo wa umeme utaongezeka na baadae kupungua (e)Mkondo wa umeme utapungua na baadae kuongezeka [ ]


38. **Vyanzo mbalimbali vya nishati zinazotumika kupikia majumbani huwa na madhara kwenye mazingira. Sababu ipi inaifanya nishati itokanayo na gesivunde kuwa nzuri kwa matumizi? ____ (a)Haitoimoshi katikauzalishaji wake (b)Inatoa gesi ya oksijeni (c)Inatoa gesi ya kabonidayoksaidi (d)Haina gharama katika uzalishaji (e)Haitumiki kwa wingi [ ]**

39. **Mwalimu alifundisha mambo mbalimbali kuhusu mabadiliko ya kiumbo. Je,ni mfano upiulitolewa na mwalimu kuelezea mabadiliko hayo? ______________________**
**(a)Kuoza kwa mimea au wanyama (b)Chuma kupata kutu (c)Kuyeyusha sukari kwenye maji (d)Kuunguza kipande cha mti (e)Kuchachuka kwa maziwa [ ]**

40. **Upi ni mpangilio sahihi wa maada kuanzia yenye kani kubwa hadi ndogo ya mvutano kati ya molekuli? ____________**
**(a)Yabisi, gesi na kimiminika (b)Kimiminika, yabisi na gesi (c)Gesi, kimiminika na yabisi (d)Yabisi, kimiminika na gesi (e)Kimiminika, gesi na yabisi [ ]**

**SEHEMU B**

41. **Chunguza Kielelezo kifuatacho kinachohusu mabadiliko ya kiumbo ya maji kisha jibu swali linalofuata**




**Kwa kutumia herufi A – D, bainisha mchakato unaosababisha mabadiliko ya hali moja kwenda nyingine kama mshale unavyoelekeza**

______________________________________________

42. **Shule ya Msingi Chechemea iliandaa mahitaji ya vifaa vya kieletroniki vinavyohitajika pamoja na gharama zake kama inavyoonekana katika mkekakazi ufuatao:-**

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Namba | Jina la kifaa | Idadi | Gharma (Tsh.) |
| 2 | 1 | Televisheni | 1 | 300,000 |
| 3 | 2 | Tarakilishi | 2 | 800,000 |
| 4 | 3 | King'amuzi | 1 | 90,000 |
| 5 | 4 | Printa | 1 | 250,000 |
| 6 | 5 | Jumla | | |

(a) **Kifaa chenye jina la "tarakilishi" kipo katika seli gani? ______________________**

(b) **Je,utatumia fomula gani kupata jumla ya gharama za vifaa vyote?______________________**

43. **Mtu anaweza kuwa na magonjwa kama pumu, kisukari, kansa na shinikizo la damu kwa muda mrefu bila kuonesha dalili zozote. Magonjwa haya kwa pamoja yana sifa gani nyingine? ______________________**

44. **.Mara nyingi,mtu mwenye maambukizi ya VVU/UKIMWI huugua kifua kikuu. Kwa nini hutokeahivyo? ____________**

45. **(a)Ni kiungo kipi hupitisha virutubisho na hewa ya oksijeni kutoka kwa mama kwenda kwa kijusiwakati wa ujauzito? ______________________**
**(b)Kwa nini mwanamke ambaye ovari zake hazifanyi kazi hawezi kushika ujauzito? ______________________**

# MAJIBU YA JARIBIO

## SOMO LA SAYANSI NA TEKNOLOJIA – DARASA LA VII

| Na | Jibu | Na | Jibu | Na | Jibu |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | 21 | | 41 | |
| 2 | | 22 | | | |
| 3 | | 23 | | | |
| 4 | | 24 | | | |
| 5 | | 25 | | 42 | |
| 6 | | 26 | | | |
| 7 | | 27 | | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 8 | | 28 | | 43 | |
| 9 | | 29 | | | |
| 10 | | 30 | | | |
| 11 | | 31 | | | |
| 12 | | 32 | | | |
| 13 | | 33 | | 44 | |
| 14 | | 34 | | | |
| 15 | | 35 | | | |
| 16 | | 36 | | | |
| 17 | | 37 | | 45 | |
| 18 | | 38 | | | |
| 19 | | 39 | | | |
| 20 | | 40 | | | |